Nipashe
MWANGA WA JAMII
Jumatatu Julai 20, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580288
www.ippmedia.com

The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



## Jela miaka 2 kwa kumtukana mama yake matusi ya nguoni

UKURASA 10




UKURASA 11

# Mbivu, mbichi wagombea CCM kesho

• **Ni** baada ya mchujo unaoanza leo, washindi waonywa kushangilia; Shein ataja sifa Zanzibar... *Endelea Ukurasa 2*

## Mtiania urais CHADEMA arejesha fomu kwa bajaji

UKURASA 4



Mgombea urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussein Mwinyi, akiwahutubia wanachama wa chama hicho na wananchi kisiwani Pemba katika uwanja wa Kibirinzi Chakechake,wakati wa mkutano wa kutambulishwa. **PICHA: IKULU**

Nipashe
MWANGA WA JAMII
Fursa kwa Wagombea! 2020
VOTE




Gazeti la Nipashe linatoa fursa kwa wagombea wote wa vyama vya siasa kunadi sera zao kupitia kurasa zetu kwa gharama nafuu.

Wasiliana nasi
The Guardian Limited
Simu: 0686 101335,
Barua pepe: advertise@guardian.co.tz



Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play
App Store

MICHEZO MWADUI YAICHONGEA MTIBWA KWA YANGA UK.23
MAONI, KATUNI UK.6




Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, akizungumza na watumishi wa Halmashauri ya Arusha, wakati Mkuu wa Mkoa wa Arusha alipofanya ziara ya kikazi katika halmashauri hiyo juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Mbivu, mbichi wagombea CCM kesho

**Na Waandishi Wetu**

MBIVU na mbichi kwa majina yatakayoteuliwa kupeperusha bendera ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), kuwania nafasi ya ubunge, udiwani/wadi na viti maalumu katika uchaguzi mkuu wa Oktoba, mwaka huu, itajulikana kesho baada ya watia nia wote waliojitokeza kujadiliwa na kuchujwa kwenye kura za maoni.

Mchujo huo unaanza leo baada ya wagombea katika kila jimbo kujieleza mmoja baada ya mwingine na kufuatia kura ya maoni kwa kila jimbo leo na kesho, kwa kupitisha majina yatakayokwenda kamati ya mkoa na baadaye taifa ili kupata jina moja la atakayegombea kwa tiketi ya chama hicho.

Mchujo huo unakuja baada ya kumalizika kwa pilikapilika za kuchukua na kurejesha fomu za ubunge, udiwani/wadi na viti maalum katika majimbo na kata mbalimbali tangu Julai 14 hadi 17, mwaka huu.

Wote waliochukua fomu na kuzirejesha, wanaomba ridhaa ya chama chao cha CCM kupeperusha bendera Oktoba, mwaka huu, huku kukiwa na utitiri wa makada waliojitokeza kwenye chama hicho.

Wiki iliyopita, Mwenyekiti wa CCM Taifa, Dk. John Magufuli, alisema zaidi ya wanachama 8,000 wamechukua fomu kuomba ridhaa ya kupeperusha bendera ya CCM, huku Mkoa wa Dar es Salaam ukiongoza kwa kuwa na wagombea wengi zaidi.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa hivi karibuni na Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Hamphrey Polepole, Julai 30, itakuwa ni vikao vya kamati za siasa za jimbo kujadili wagombea na kutoa mapendekezo kwa kamati ya siasa za wilaya.

Agosti mosi na 2, vikao vya kamati za siasa za wilaya vitafanyika kwa ajili ya kuwajadili wagombea na kutoa mapendekezo yake kwa kamati za siasa mkoa.

Ratiba hiyo ilionyesha kuwa Agosti 4 na 5, vikao vya kamati za siasa za mkoa, vitakaa kuwajadili wagombea na kutoa mapendekezo kwa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa kwa Tanzania Bara.

Pia, kwa upande wa Zanzibar kutoa mapendekezo kwa kamati maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa Zanzibar.

Kwa mujibu wa ratiba hiyo, Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi, vikao vyake vitaanza kesho na keshokutwa kwa mikutano mikuu ya CCM ya majimbo/wilaya, kupiga kura za maoni za wagombea wa ubunge na ujumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Julai 30, kutakuwa na vikao vya kamati za siasa za CCM za jimbo kuwajadili wagombea na kutoa mapendekezo kwa kamati za siasa wilaya.

Vikao vya kamati za siasa wilaya vitakaa Agosti mosi na 2, kuwajadili wagombea na kutoa mapendekezo kwa kamati za siasa mikoa, huku vikao vya kamati za siasa mikoa vitawajadili wagombea na kutoa mapendekezo yake Agosti 4 na 5, mwaka huu. Kwa upande wa Viti Maalum, Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) na Umoja wa Wazazi Tanzania, mchakato wao utafanyika kwa mikutano ya Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) ya mikoa kupiga kura ya maoni kwa wagombea wa viti vya mkoa na makundi mengine isipokuwa kundi la vijana na wazazi.

Julai 30, Baraza la Vijana la mkoa litapiga kura za maoni kwa wagombea wa viti maalum kundi la vijana.

Agosti 31, Baraza la Wazazi la mkoa litapiga kura za maoni kwa wagombea wa viti maalum kundi la wazazi.

Agosti 4 na 5, kamati za siasa za CCM za mikoa zitatoa mapendekezo yake yatakayowasilishwa kwenye Baraza Kuu la UWT Taifa.

Agosti 8, mwaka huu, Baraza Kuu la UVCCM litapiga kura za maoni kwa wagombea wa ubunge na uwakilishi viti maalum (kundi la vijana).

Agosti 9, Baraza Kuu la Wazazi litapiga kura za maoni kwa wagombea wa ubunge na uwakilishi viti maalum (kundi la vijana).

Agosti 10, Baraza Kuu la UWT litapiga kura za maoni kwa wagombea wa ubunge na uwakilishi viti maalum na kuandaa mapendekezo yakatayowasilishwa kwenye Halmashauri Kuu ya Taifa.

Kwa upande wa udiwani/wadi, Julai 25, mwaka huu, kutakuwa na mkutano mkuu wa UWT, ngazi ya wilaya kwa ajili ya kura za maoni.

Pia, Julai 27, mwaka huu, kutakuwa na mkutano mkuu wa CCM ngazi ya kata/wadi kwa ajili ya kura za maoni kwa nafasi za udiwani.

Pia, Julai 29, mwaka huu itakuwa ni vikao vya kamati za siasa za CCM kata/wadi kuwajadili wagombea na kutoa mapendekezo yake kwa kamati za siasa za jimbo (Zanzibar) na wilaya kwa upande wa bara.

Kwa mujibu wa ratiba hiyo, Julai 30,mwaka huu, ni vikao vya kamati za siasa za CCM za jimbo Zanzibar kuwajadili wagombea na kutoa mapendekezo yake kamati za siasa wilaya.

Agosti mosi, itakuwa siku ya vikao vya kamati za siasa za CCM za wilaya kuwajadili wagombea na kutoa mapendekezo kwa kamati za mikoa.

Kuanzia Agosti 4 hadi 5, itakuwa ni siku ya vikao vya kamati za siasa za mikoa kuwajadili wagombea na kutoa mapendekezo yake kwa kamati za siasa za mkoa.

Ratiba hiyo ilionyesha kuwa kwa ngazi hiyo Halmashauri Kuu itakutana Agosti 6 na 8, kwa ajili ya uteuzi wa mwisho.

**WATAKAOSHINDA WAONYWA**

Katibu wa Oganaizesheni, Pareira Silima, alisema waliojitokeza kwa ubunge na viti maalum ni makada zaidi ya 10,000, na kuwataka wanachama kudumisha amani na utulivu.

Alisema matokeo ya kura za maoni sio uamuzi bali ni taarifa kwa ajili ya uamuzi, na kuwaonya watakaoibuka na ushindi wasishangilie. Pia aliwataka wasimamizi kutenda haki kwa kuhakikisha kura zinahesabika papo hapo na kwa uwazi.

**Imeandikwa na Salome Kitomari, DAR na Agusta Njoji, DODOMA**


**KUPOTEA KWA CHETI**



TEGEMEA CHRISTOPHER MANDELE anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba P1099/0017 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia NYEHUNGE SEKONDARY SCHOOL CENTER mwaka 2014.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi: DAR/OST/RB/536871/2020.

158171


# Shein ataka sura mpya Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAKATI Chama cha Mapinduzi (CCM) leo kinaanza vikao vyake vya kuwachuja wanachama wa chama hicho waliochukua fomu ya kugombea nafasi za ubunge, uwakilishi na udiwani, Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amefurahishwa na sura mpya zilizojitokeza ambao wengi wao ni vijana kugombea nafasi hizo.

Alitaka wachaguliwe wale wenye sifa ambao wataendana na kasi ya mgombea wa urais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi.

Dk. Shein aliyasema hayo jana wakati akimtambulisha Dk. Mwinyi katika viwanja vya Tibirinzi Kisiwani Pemba.

Alisema kuwa anataka kuona sura zengine za wawakilishi, wabunge na madiwani na sio sura hizo hizo katika nafasi hizo.

"Chaguweni viongozi wazuri na sio wababaishaji wenye tamaa, tunataka viongozi wenye uwezo wanaowavutia wapigakura," alisema Dk. Shein, ambaye pia ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la mapinduzi.

Dk. Shein aliongeza kwa kusema kuwa:"Hatutaki kuona sura hizo hizo miaka yote na wala hatutaki shikamoo."

Alieleza kuwa wakichagua viongozi hao hao ambao wameshaongoza majimbo kwa miaka mingi itakuwa kama bei ya pilipili kichaa ilivyokuwa miaka ya nyuma, ambayo haikubadilika kwa kipindi hiki.

Aliwataka viongozi wa CCM katika mchujo huo wa kutafuta wagombea wawajadili kama Kamati Kuu ya CCM ilivyojadili wagombea urais wa Zanzibar na hatimae akapatikana Dk. Mwinyi.

Alieleza kuwa ushindi CCM ni lazima, hivyo ni vyema kupata viongozi wenye uwezo, upeo na wenye mvuto kwa wapigakura.

Aidha, Dk. Shein alisema kuwa amefurahishwa kuona mapokezi makubwa kisiwani Pemba, na kuwataka wananchi wa Pemba kumpa ushirikiano mgombea huyo.

**KAULI YA DK. MWINYI**

Naye mgombea urais, Dk. Hussein Mwinyi, alisema kuwa endapo atapata ridhaa ya wananchi, atahakikisha anadumisha amani kwa sababu bila ya amani maendeleo hayapatikani.

Alisema pia kipaumbele chake kingine ni kudumisha umoja, mshikamano na kutokuwa na ubaguzi wa upemba na uunguja katika fursa mbalimbali yakiwamo masuala ya ajira.

Alisema atahakikisha maslahi bora kwa kila Mzanzibari na lazima watu wawajibike, maana bila ya uwajibikaji, maendeleo hayataweza kupatikana.

Dk. Mwimyi alirejea kauli yake ya kuwa wapo wanaomuona yeye ni mpole, lakini watamuelewa kwa kuwa hatawafumbia macho wala rushwa, wabadhirifu na wahujumu wa uchumi.

Alieleza kuwa katika uchaguzi wa mwaka huu, CCM itapata ushindi wa kishindo usio na malalamiko.

Kadhalika, alisema anashangazwa na kauli kutoka kwa baadhi ya watu kuwa waliojitokeza kugombea nafasi za uongozi majimboni kupitia CCM amewatuma ili apate kuwateua katika baraza la mawaziri.

"Mimi sijamtuma mtu akagombee ili nimteuwe katika baraza langu la mawaziri... kamanitakua rais wa Zanzibar nasema kila mmoja kupambana na hali yake," alisema.

Katika mapokezi hayo yaliyoanzia uwanja wa ndege Chake Chake Pemba hadi viwanja vya Tibirinzi wananchi walifurika huku Pemba iking'ara kwa rangi za kijani na njano.

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, akichanganya zege la ujenzi wa bwalo la Shule ya Sekondari ya Mwanhala wakati wa ziara yake wilayani Nzega ya kukagua miradi ya maendeleo jana.
**PICHA: VINCENT TIGANYA**

# Membe arejesha fomu ya urais

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa zamani wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Bernard Membe, jana alirejesha fomu ya kuomba kuteuliwa na Chama cha Act-Wazalendo kuwania nafasi ya urais katika uchaguzi mkuu mwaka huu.

Waziri huyo wa zamani alijiunga na chama hicho Julai 8, mwaka huu akitokea Chama Cha Mapinduzi (CCM), ambako alifukuzwa tangu Februari, mwaka huu kwa tuhuma mbalimbali ikiwamo kukiuka kanuni na miongozo ya chama chake hicho cha zamani.

Membe alifukuzwa na kikao cha Kamati Kuu, lakini Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM iliridhia uamuzi huo hivi karibuni jijini Dodoma wakati wa vikao vya mchakato wa kuwateua na kuwathibitisha wagombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar.

Membe alirejesha fomu hiyo katika ofisi za chama hicho zilizopo Magomeni, Dar es Salaam na kupokelewa na Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho Bara, Joran Bashange.

Membe alirejesha fomu hiyo ikiwa ni siku moja tu baada ya kuichukua siku ya Ijumaa iliyopita.

Membe ndiye mgombea wa kwanza na wa pekee katika nafasi hiyo aliyejitokeza kuchukua na kurudisha fomu ya kuwania nafasi ya kupeperusha bendera ya ACT-Wazalendo katika uchaguzi huo mkuu wa Oktoba.

Akizungumza na Nipashe, Naibu Katibu Uenezi, Habari na Mahusiano kwa Umma wa chama hicho, Janeth Rithe, alithibitisha Membe kurejesha fomu hiyo ikiwa imekamilika.

# Matukio ya moto yalishtua Jeshi la Polisi

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi nchini limesema litachukua hatua kali kwa vyuo, shule au taasisi zitakazobainika kukiuka maelekezo ya kisheria katika kujikinga na kuepuka majanga ya moto.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, David Misime, taasisi hizo zinapaswa kufuata kanuni na taratibu zilizopo ili kuepuka madhara hayo.

Alisema ni wajibu wa kila mmiliki na viongozi wa shule kuendelea kuchukua tahadhari na kuhakikisha wanafanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa kuwatumia wataalam wa masuala la moto. Vile vile, alisema ukaguzi huo unafanyika kama taratibu na kanuni zinavyoelekeza kwa majengo ya taasisi za elimu na utafiti, ikiwa ni pamoja na kuzingatia suala la ulinzi.

Misime alirejelea matukio ya hivi karibuni ya Julai 4 na 17, mwaka huu, kwa Shule ya Sekondari Ilala Islamic kuungua kwa moto na kusababisha vifo vya wanafunzi watatu na uharibifu mkubwa wa mali.

Pia, tukio jingine ni la Shule ya Sekondari ya Kinondoni Muslim na tukio la Julai 18, mwaka huu, Shule ya Sekondari ya Mivumoni Islamic kwa darasa moja kuteketea kwa moto.

“Matukio haya ni wazi kuwa yameleta taharuki na maswali mengi kwa jamii kuhusiana na namna matukio yanayojitokeza kwa mfululizo,” alisema na kuongeza:

“Vyombo vya dola vinaendelea kufanya uchunguzi ili kuweza kubaini vyanzo vya moto huo vilivyosababisha vifo, hofu kwa wafanyakazi, wanafunzi, wazazi/walezi pamoja na kusababisha harasa kubwa.”






Mmoja wa vijana waliopata mafunzo ya kilimo cha biashara, Telesia Ngumbi kutoka mkoani Iringa, akitoa maelezo ya elimu aliyoipata ya kilimo hicho kwa Mratibu wa Kitaifa wa Mkakati wa Vijana kushiriki katika kilimo kutoka Wizara ya Kilimo, Levilian Ngaiza (Mwenye suti). **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# Mtiania urais CHADEMA arejesha fomu kwa bajaji

**Na Elizabeth Zaya**

WATIANIA saba kati ya 11 waliokuwa wamechukua fomu za kuomba uteuzi wa kugombea urais kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wamerejesha fomu hizo, huku mmoja akitumia pikipiki ya miguu mitatu (bajaji) kuwahi kuirejesha.

Jana ndiyo ilikuwa siku ya mwisho kwa watia nia ya urais ndani ya CHADEMA kurejesha fomu hizo.

Aliyetumia bajaji kuwahi kurejesha fomu hizo ni Dk. Maryrose Majinge, ambaye alikuwa ameongozana na msaidizi wake, ambaye naye alikuwa mwanamke akiwa amembebea mkoba.

Baada ya kuwasili katika ofisi hizo, alipokelewa na wanachama wa chama hicho na baadhi ya viongozi waliokuwa katika ofisi hizo.

Akizungumza baada ya kukabidhi fomu zake za kuomba kuteuliwa kupeperusha bendera ya chama hicho kwa nafasi ya urais, Dk. Majinge alisema matumani yake ni kuingia Ikulu.

"Matumaini yangu ni kuingia Ikulu kwa sababu chama changu kimejipanga vya kutosha na nataka niwaambie Watanzania kwamba chakula walichokuwa wakikisubiri sasa kimeiva, kilichobaki ni kukitenga tu mezani," alisema Dk. Majinge.

Aliwashukuru wanachama wa chama hicho waliojitokeza kumdhamini nchi nzima. "Nishukuru wanachama wenzangu nchi nzima kwa kuniamini na kunidhamini na hatimaye nimekamilisha mchakato wa kujaza fomu na kuzirudisha, niombe tu kwamba Watanzania wasiogope kwa sababu tupo tayari kuwatumikia," alisema Dk. Majinge.

Mbali na Dk. Majinge, wengine walionekana kurejesha fomu hizo ni Mwenyekiti wa Chama hicho Kanda ya Nyasa, Lazaro Nyalandu, ambaye alirusha taarifa kupitia akaunti yake ya Instagram ikimuonyesha akikabidhi fomu hizo na kuandika kwamba alikuwa akizirejesha.

**WENGINE WALIOREJESHA**

Katika akaunti yake hiyo, Nyalandu aliandika "Nikirejesha fomu" aliandika kwa kifupi huku picha yake ikionekana akikabidhi.

Hata hivyo, Mkuu wa Idara ya Mawasiliano wa CHADEMA, Tumaini Makene, alipotafutwa kwa ajili ya kufahamu idadi ya watiania waliorejesha fomu hizo, hakupokea simu, ingawa taarifa za ndani ambazo Nipashe ilizipata, zilieleza kwamba mpaka saa kumi jioni jana, wengine waliokuwa wamerejesha ni Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Tundu Lissu.

Mwingine ni aliyekuwa Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Isaya Mwita, Wakili Simba neo, Leonard Manyama na Gasper Mwanalelya.

Idadi ya waliochukua fomu za kuomba kuteuliwa ilikuwa 11, akiwamo Mwenyekiti wa Chama hicho, Freeman Mbowe, Peter Msigwa na Msafiri Shaban ambao kwa mujibu wa taarifa hizo za ndani, mpaka pazia hilo linafungwa jana walikuwa hawajarejesha.

**KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI**

**TANZANIA CHINA DEVELOPMENT LTD** inatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba ya usajili **MC738 CKF** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania . Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochcote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DOD/KON/533493/2020**

# Jafo ataka Watanzania kudumisha amani

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, amewataka Watanzania kuendelea kudumisha amani wakati wa uchaguzi mkuu, kwamba ni ajenda muhimu kuliko kitu chochote.

Amesema uzalendo wa kulinda amani ndiyo jambo la kwanza nchini, hivyo kila Mtanzania ana wajibu wa kuhakikisha anailinda amani wakati wote.

Alitoa rai hiyo jijini Dar es Salaam wakati akizindua duka kubwa la kuuza mahitaji ya nyumbani liitwalo 'Smart Buy Hypermarket' na kutoa angalizo kwa Watanzania wakati wa uchaguzi.

"Angalieni Libya ya sasa siyo ile ya zamani, sasa hivi wanaishi kama wakimbizi, amani imetoweka, bila amani huwezi kufanya biashara wala kitu chochote. Hivyo ndugu zangu nawasihi tujali amani kwanza kuliko mtu," alisema Jafo.

Jafo aliongeza: "Tunapaswa tujivunie na nchi yetu, tuungane na Rais John Magufuli katika kuijenga nchi. Rais Magufuli anatengeneza mazingira rafiki ili uchumi ukue, anataka wawekezaji wawekeze vizuri ndiyo maana anaweka mazingira rafiki." Jafo alisema Rais Magufuli alitenga Sh. trilioni 1.2 kwa miaka mitano kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu, ikiwamo Sh. bilioni 600 kujenga miundombinu katika Jiji la Dar es Salaam. "Kama mnakumbuka tulinyimwa pesa za MCC mwaka 2015, lakini leo vijiji zaidi ya 9,000 vina umeme wakati awali vijiji vilivyokuwa na umeme vilikuwa 2,000 tu," alisema Jafo.

Kuhusu duka hilo, Jafo alisema uwekezaji uliofanyika ni mojawapo ya kuinua uchumi wa nchi kwa kuwa bidhaa zinazouzwa zinazalishwa na Watanzania.

"Mlichokifanya hapa ni kujivunia na nchi yenu, mtu akinunua bidhaa za ndani inaongeza ukuaji wa uchumi. Nawasihi wafanyakazi muwe na nidhani katika kazi," alisema Jafo.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Smart Buy-Hyper Market, Rajab Khamis, alisema uwekezaji uliofanyika katika duka hilo ni zaidi ya Sh. bilioni 100, lina wafanyakazi zaidi ya 40 ambao wote ni Watanzania.

Alisema wajasiriamali wadogo wanakaribishwa kuleta bidhaa zao na kwamba zitanunuliwa kwa bei nzuri.

**KUPOTEA KWA CHETI**



**CASTORY NICOLOUS MATIMBWI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato ch nne chenye **index namba S2655/0092** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2019 katika shule ya Sekondari Maranatha. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **MBE/MBA/RB/507359/2020.**

# Afariki kwa kupondwa jiwe kichwani akichimba madini

**Na Mohab Dominick,**
SHINYANGA

MKAZI wa Kijiji cha Masungura wilayani Meatu, Simiyu Michael Salum (30), amefariki dunia kwa kupondwa na jiwe kichwani wakati akichimba dhahabu ndani ya duara katika machimbo ya Mwakitolyo, wilayani Shinyanga.

Ofisa Madini Mkoa wa Shinyanga, Joseph Kumburu, akizungumza hivi karibuni na wachimbaji wadogo wa Mwakitolyo, alisema kuwa tukio hilo limetokea Julai 17, mwaka huu na kuwa ajali hiyo ilitokea katika kitalu cha wachimbaji wadogo wa namba 5. Kumburu alisema ajali hiyo imetokea majira ya saa 6:00 mchana wakati wachimbaji zaidi ya watano walipokuwa wakitoka ndani ya duara baada ya kumaliza kazi.

Kumburu alisema, kwa mujibu wa Mtaalam wa afya aliyekuwa kwenye uchunguzi huo, mtu huyo alipasuka kichwani na kusababisha umauti kutokana na kuanguka kutoka umbali wa mita 20, baada ya kuteleza na jiwe kumponda kichwani na kusababisha kifo chake.

"Marehemu hakuwa na majeraha yoyote zaidi ya kupasuka kichwa, niwashauri tu ndugu zangu wachimbaji muhakikishe mnazingatia taratibu na sheria za uchimbaji mnazoelekezwa na wataalamu wenu ili kufanya shughuli hizo kwa hali ya usalama zaidi kwa kuwa chanzo cha tukio marehemu alikosa nguvu," alisisitiza Kumburu.

Kutokana na ajali za mara kwa mara zinazotokea kwenye machimbo hayo, Ofisa Madini huyo alifunga eneo kulipotokea ajali kwa siku tatu kupisha ukaguzi. Kumburu aliandaa timu ya wataalam kutoka Ofisi ya Madini, kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Salawe pamoja na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Shinyanga ili kusimamia ukaguzi huku akishauri hatua za haraka za kuchukuliwa kwa maduara yote yatakayobainika kuhatarisha maisha ya watu.

Ofisa Madini Kumburu aliwataka wachimbaji hao kuzingatia Sheria za madini na maelekezo wanayopewa na wakaguzi kufukia mashimo yote ambayo yameachwa wazi ili kuepusha ajali.

## TANGAZO

tigo pesa

# Ni Zaidi ya Pesa

## Ada za wateja. Piga *150*01#

| Kiwango (Tsh) | | Ada kwa mteja (Tsh) | | |
|---|---|---|---|---|
| Kuanzia | Mwisho | Kutuma pesa kwenda Tigo Pesa | Kutuma pesa kwenda Mitandao washirika | Kutoa pesa kwa Wakala/ATM |
| 100 | 999 | 15 | 15 | N/A |
| 1,000 | 1,999 | 30 | 50 | 300 |
| 2,000 | 2,999 | 30 | 50 | 400 |
| 3,000 | 3,999 | 50 | 100 | 600 |
| 4,000 | 4,999 | 60 | 100 | 650 |
| 5,000 | 6,999 | 130 | 200 | 950 |
| 7,000 | 9,999 | 150 | 200 | 1,000 |
| 10,000 | 19,999 | 360 | 550 | 1,450 |
| 20,000 | 29,999 | 380 | 600 | 1,850 |
| 30,000 | 39,999 | 400 | 680 | 1,850 |
| 40,000 | 49,999 | 410 | 750 | 2,350 |
| 50,000 | 99,999 | 720 | 1,250 | 2,700 |
| 100,000 | 199,999 | 1,000 | 1,600 | 3,650 |
| 200,000 | 299,999 | 1,200 | 1,900 | 5,300 |
| 300,000 | 399,999 | 1,500 | 2,300 | 6,500 |
| 400,000 | 499,999 | 1,500 | 2,500 | 7,000 |
| 500,000 | 599,999 | 2,200 | 3,200 | 7,500 |
| 600,000 | 799,999 | 3,300 | 4,300 | 8,000 |
| 800,000 | 899,999 | 3,500 | 4,300 | 8,000 |
| 900,000 | 1,000,000 | 3,500 | 6,000 | 8,000 |
| 1,000,001 | 3,000,000 | 5,000 | 6,000 | 8,000 |
| 3,000,001 | 10,000,000 | 5,000 | 6,000 | 10,000 |

| Tukio | Kuanzia | Mwisho | Ada |
|---|---|---|---|
| Kuweka pesa | 1,000 | 5,000,000 | BURE |
| Kutuma pesa kwa mteja ambaye hana akaunti ya Tigo Pesa au akaunti ya mitandao washirika | 1,000 | 1,000,000 | Ada ya kutuma + Ada ya kutoa |
| Kutoa pesa kwa mteja ambaye hana akaunti ya Tigo Pesa au akaunti ya mitandao washirika | 1,000 | 1,000,000 | BURE |
| Kutuma pesa kwenda nchi za nje | 100 | 5,000,000 | Kulingana na kiwango |
| Malipo kwa Tigo Pesa | 500 | 5,000,000 | Kulingana na kiwango |

| Tukio | Ada |
|---|---|
| Kubadilisha namba ya siri | BURE |
| Kuangalia salio/ Taarifa ndogo | 50 |
| Kurudisha muamala uliokosea (Jihudumie) | 50 |
| **Kupata taarifa ya mwezi** | **Ada** |
| Taarifa ya Mwezi jana/Mwezi huu | BURE |
| Taarifa ya Miezi 3 | 1,000 |
| Taarifa ya Mwaka 1 | 2,000 |

Kwa vigezo na masharti ya huduma tembelea tovuti: https://www.tigo.co.tz/tigo-pesa-standard-terms-and-conditions. **Ada zote zimejumuisha kodi zote zinazohusika**
Kwa Ada za huduma nyingine tembelea tovuti; **https://www.tigo.co.tz/tigo-pesa-tariffs**

**Furahia Malipo kwa Tigo Pesa:**


**KUMBUKA:**
1. Unaweza kuweka au kupokea hadi TSh 5,000,000 kwa siku na unaweza kutoa au kutuma hadi TSh 5,000,000 kwa siku, pia unaweza kuhifadhi hadi TSh 10,000,000 kwa wakati mmoja kwenye akaunti yako ya Tigo Pesa, kama usajili wako umekamilika.
2. Onesha kitambulisho chako kabla ya kuweka au kutoa pesa kwa Wakala.
3. Hakikisha taarifa zako za usajili ni sahihi kwa kupiga *106# kisha 2 au piga huduma kwa wateja kwa maelezo zaidi.
4. Hesabu pesa zako na hakikisha salio lako la Tigo Pesa linaendana na muamala uliofanya kabla ya kuondoka kwa Wakala.
5. Kila mara unapotuma pesa, kumbuka kuhakiki namba ya mpokeaji kuepuka kukosea na usumbufu.
6. Hakikisha unahifadhi namba yako ya siri (PIN) kwa usalama. Usimpe wala kumtajia mtu yeyote namba yako ya siri; iwe wakala wa Tigo Pesa, mfanyakazi wa Tigo au mhudumu wa Tigo Huduma kwa Wateja. Pia kumbuka kubadili namba yako ya siri mara kwa mara.
7. Kutuma muamala wa zaidi ya TSh 5,000,000 ni kwa wafanyabiashara waliosajiliwa pekee.
8. Tigo itakupigia kwa 0713800800 au 0713123103 Tu.
9. Kutoa taarifa yoyote dhidi ya udanganyifu Piga simu namba 100 au tuma ujumbe kwa barua pepe kwenda customercare@tigo.co.tz
10. Unaweza kupokea pesa kutoka zaidi ya Nchi 150 duniani

Unaweza kurudisha **muamala uliokosea**, **token ya luku**, **ku-unbar akaunti yako ya Tigo Pesa** na **kuriseti PIN**

Piga ***150*01#**
chagua **6 (Jihudumie)**
kisha chagua huduma unayotaka

tigo pesa

App yenye urahisi wa kushangaza!




**Fanya malipo ya Serikali**

SUMATRA
TANESCO LUKU

Pakua kwenye
Google Play
App Store

tigo pesa

Kuwasaliana na huduma kwa wateja,
Piga **100** bure au tembelea duka lolote la Tigo!
Ada hizi ni kuanzia June 2020

tigo

www.tigo.co.tz

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## TFF iongeze umakini lala salama Ligi Kuu

**HATIMAYE** Ligi Kuu Bara itafikia ukingoni Jumapili wiki hii baada ya kupitia kipindi kigumu ikiwa ni pamoja na kusimama kwa miezi miwili na wiki mbili kabla ya uamuzi wa serikali kuruhusu ligi nchini kuendelea na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) pamoja na Bodi yake ya Ligi (TPLB) kuirejesha Juni 13, mwaka huu.

Ligi hiyo ambayo awali ilisimama tangu Machi 17, mwaka huu kutokana na mlipuko wa maambukizi ya virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19, wakati huo zikiwa zimebaki mechi 10 kabla ya msimu kumalizika, kwa sasa kila timu imebakiza mechi mbili tu kuelekea ukingoni mwa msimu huu wa 2019-20202 na tayari mabingwa watetezi, Simba wameshautwaa ubingwa huo ikiwa ni mara ya tatu mfululizo.

Hata hivyo, bado kuna kinyang'anyiro kikali katika kuwania kumaliza nafasi ya pili kati ya Yanga na Azam FC ambayo jana ilishuka dimbani ugenini mjini Iringa dhidi ya Lipuli, kucheza mechi yake ya 36. Yanga ambayo tayari imeshashuka dimbani mara 36, ipo nafasi ya pili ikiwa na alama 68 tatu mbele ya Azam ikifuatiwa na Namungo FC yenye pointi 64 zilizotokana na michezo 36, hivyo nayo huwezi kuitoa katika kinyang'anyiro hicho endapo timu hizo mbili zitateleza.

Mbali na kinyang'anyiro hicho, kazi kubwa ipo katika ukanda wa kushuka daraja ambapo msimu huu zitapanda timu mbili moja kwa moja huku zikishuka nne, na mbili kutoka Ligi Kuu zikitakiwa kucheza mechi za mchujo na timu za Daraja la Kwanza ili kuwania nafasi mbili ya kucheza ligi hiyo ya juu nchini.

Hiyo ni kutokana na TFF kuamua kuiboresha Ligi Kuu kwa kupunguza timu hadi kufikia 18 msimu ujao wa 2020-2021 kabla ya msimu wa 2021-2022 kuzifyeka tena na kubaki 16 tu.

Kabla ya mechi za jana, msimamo unaonyesha timu zilizopo salama kubaki Ligi Kuu msimu ujao, ni nane tu; mabingwa Simba, Yanga, Azam, Namungo, Polisi Tanzania, Coastal Union, Kagera Sugar na JKT Tanzania, huku nafasi ya Biashara United na Ruvu Shooting zenye alama 47 bado zikiwa mashakani kutokana pointi hizo kuweza kufikiwa na timu zilizopo nyuma yao endapo zitapoteza michezo yao miwili ya mwisho na wapinzania wao kushinda.


Singida United yenye pointi 18, tayari imeshuka daraja huku Mbao FC, Lipuli FC, Ndanda, Alliance iliyoshuka dimbani jana dhidi ya Simba pamoja na Mwadui FC zikiwa katika ukanda mbaya wa kuweza kuungana na vibonde hao wa kwanza kuaga Ligi Kuu. Huu unaonyesha ni moja kati ya misimu migumu zaidi kuwahi kutokea katika Ligi Kuu Bara, kwa zaidi ya timu sita kuwa katika nafasi ya kushuka daraja wakati zikiwa zimesalia raundi mbili kabla ya msimu kumalizika.

Tunatambua tayari wawakilishi wa Tanzania katika michuano ya kimataifa wameshajulikana, ambapo Simba kwa kutwaa ubingwa itapeperusha bendera ya Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa wakati Namungo FC ikiiwakilisha nchi Kombe la Shirikisho Afrika baada ya kufanikiwa kutinga fainali ya Kombe la FA sambamba na Simba yenye tiketi ya michuano ya kimataifa mkononi. Hivyo, tunachoitaka TFF pamoja na TPLB kwa sasa ni kuongeza umakini zaidi katika lala salama hii ya Ligi Kuu kwa kumulika ukanda wa timu zinazowania kuepuka kushuka daraja ili kutopanga matokeo kwenye michezo hii ya raundi hizi mbili za mwisho.

Lengo leo ni kutaka kuona timu zinazobaki Ligi Kuu msimu ujao zinapata nafasi hiyo kihalali kutokana na ubora wao uwanjani na si kwa njia ya kubebwa ama kwa kupitia waamuzi au kununua mechi kwa timu ambazo tayari zipo katika ukanda salama.

Tunaamini kama TFF kupitia TPLB itatekeleza hilo, kutaifanya Ligi Kuu msimu ujao kuwa na ushindani zaidi jambo ambalo litavutia wawekezaji wengi kujitokeza na kuinua uchumi wa klabu zetu lakini pia kufungua milango ya wachezaji kupata fursa ya kwenda kucheza soka la kulipwa nje ya nchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

### Yanga wasilaumiane, wajipange msimu ujao

**MSIMU** ujao klabu kongwe ya Yanga haitoiwakilisha Tanzania kwenye michuano yoyote ile ya kimataifa, kutokana na kuukosa ubingwa na kama vile haitoshi kuchapwa mabao 4-1 na watani zao wa jadi Simba, ikitolewa kwenye harakati za kusaka tiketi ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Hali hii imezua mtafaruku kwa baadhi ya wanachama na mashabiki wa Yanga na hasa baada ya kuchapwa mabao 4-1 dhidi ya Simba, Jumapili ya Julai 12 kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Kila mtu anaongea lake. Kuna wanaoulaumu uongozi. Wapo wanaolaumu wachezaji. Wengine nao wanamlaumu mtu mmoja mmoja, hasa mchezaji wao aliyekuwa tegemeo na kipenzi, Mghana Bernard Morrison.

Inavyoonekana ni kama viongozi wa Yanga nao wameingia kwenye mtego huo na kuanza kulalamika na kumlaumu Morrison, wakati ni wao wenyewe ndio waliyempa kiburi hicho.

Ni mchezaji ambaye baada ya kuonekana ana uwezo mkubwa wa hali ya juu, alianza kupewa malezi tofauti na wenzake. Kila anachofanya alikuwa anachekewa, kwa sababu tu 'anaupanda mpira'. Mchezaji huyo akaifunga Simba kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga ikashinda bao 1-0.

Morrison akaendelea kudeka, huku viongozi wakimdekeza anavyotaka. Kuna wakati walionekana kama wamemchoka, lakini ghafla ikaja mechi ya Simba dhidi ya Yanga, baada ya timu hizo kushinda mechi zao za robo fainali ya Kombe la FA.

Viongozi wa Yanga wakajua kabisa kuwa mkombozi wao anaweza kuwa Morrison kwa mara nyingine.

Kukariri kwao ndiko kulikofanya kumrudisha tena kundini. Tena wakamsafirisha kabisa kumpeleka mkoani Kagera ilipocheza dhidi ya Kagera Sugar na akafunga bao pekee, lililowafanya viongozi hao kuona walichofanya ni sahihi.

Kituko kilikuwa kwenye mechi dhidi ya Simba, alipotolewa mchezaji huyo na kutoka moja kwa moja nje na hakuonekana tena.

Sijajua kama angekuwa amefunga goli na Yanga ikashinda akafanya kama alivyofanya angesakamwa hivi. Nadhani hii inatokana na Yanga kupoteza mechi hiyo, ndiyo maana gunia la misumari limemuangukia Morrison ambaye ndiye aliyepewa jukumu la kuiangamiza Simba.

Hayo yote yamepita, binadamu siku zote hujifunza kutokana na makosa. Baadhi ya makosa ambayo viongozi wa Yanga waliyafanya msimu huu ni kufanya usajili kwa mihemko.

Nakumbuka wakati msimu unaanza ilikuwa na wachezaji kama kina Juma Balinya, Urkhob Sadney, Issa Bigirimana, Mustapha Selemani na wengine wengi ambao waliachwa kwenye dirisha dogo na kusajiliwa wengine kama kina Yikpe Gnamien, Morrison mwenyewe, Ditram Nchimbi, Tariq Seif na wengineo ambapo hakukuwa na tofauti kubwa kati ya walioondoka na waliopo.

Nafikiri viongozi wa Yanga walifanya haraka sana kuwaondoka kina Balinya kwenye dirisha dogo. Wangekuwa wavumilivu, huenda Yanga isingekuwa kama hivi ilivyo leo, ambapo mashabiki wengi wanalalamika kuwa kikosi hakipo vizuri msimu huu.

Nakumbuka kikosi kile cha kina Sadney, nusura kitinge hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa kama si kufungwa na Zesco ya Zambia mabao 2-1 ugenini, tena kwa bao la Yanga kujifunga wenyewe kupitia kwa Abdulaziz Makame. Na hii ni baada ya kutoka sare ya bao 1-1 nchini Tanzania, tena Zesco wakipata bao dakika za majeruhi.

Ukiangalia kikosi kile cha mzunguko wa kwanza kilionekana ni bora zaidi, lakini ulikosekana uvumilivu tu kwa baadhi ya viongozi wa Yanga.

Cha kufanya sasa si kulaumiana, wala kutumia nguvu nyingi kumlaumu Morrison au kujibizana naye, badala yake kuanza taratibu kujipanga kwa msimu ujao wa Ligi Kuu ambao sina shaka utakuwa mgumu zaidi kuliko huu unaomalizika.

Badala ya kutumia muda mwingi kulalamika, viongozi wa Yanga wangetumia muda huu kuanza kusaka wachezaji bora ambao watakuja kukiongezea nguvu kikosi.

Kama alivyosema mchezaji wa zamani wa klabu hiyo, Boniface Ambani kuwa Yanga inahitaji wachezaji bora wachache ili kufanya timu kuwa yenye ushindani na si kuwa na wachezaji wengi ambao uwezo wao ni mdogo.

Ambani akasema kuwa Yanga si lazima isajili wachezaji 30, bali hata 25 tu na hiyo pesa ya watano iliyobaki, iongezwe kwenye kupata wachezaji wenye thamani na uwezo mkubwa. Naungana na Ambani kuwa Yanga isipangue kikosi chote kwa hasira na kusajili wachezaji wengi wapya la hasha.

# Wazazi wadaiwa kupuuza kununulia watoto barakoa

**Na Zuwena Shame,** IRAMBA

SUALA la wanafunzi kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa corona kwa kuvaa barakoa katika shule nyingi limekuwa tatizo licha ya agizo la serikali kutolewa mapema mwezi ulipita kabla ya kufunguliwa shule.

Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilitoa mwongozo unaowataka wanafunzi wote (sipokuwa chini ya mika minane na wenye matatizo ya kiafya) kurejea shuleni na kuvaa barakoa kama njia mojawapo ya kijikinga na maambukizi ya ugonjwa wa corona.

Njia zingine ni kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni au kitakasa mikono.

Vilevile kukaa umbali wa mita moja baina ya wanafunzi na mwanafunzi.

Uchunguzi wa Nipashe ulibaini katika shule za msingi na sekondari wilayani Iramba, mkoani Singida, asilimia kubwa ya wanafunzi hawakuwa na barakoa. Kwa mujibu wa baadhi ya wanafunzi walidai kuwa hali za wazazi wao kiuchumi sio nzuri na hivyo kushindwa kuwanunulia barakoa.

Wakiongea na Nipashe wilayani humo, baadhi ya walimu walikiri kuwa wanafunzi wengi waliowauliza sababu ya kutovaa barakoa ni wazazi wao kutokuwa na uwezo wa kuwanunulia.

Ofisa elimu (msingi) Chacha Kehogo, alisema kwa muda wa wiki mbili tangu kufungua shule katika wilaya hiyo asilimia 99 ya wanafunzi walikuwa hawana barakoa kutokana na mwamko mdogo wa wazazi ambao wengi wao wanadai kuwa na kipato duni.

Kehogo alisema kuwa wazazi wengi wana dhana ya kuwa barakoa ni gharama na ni kwa ajili ya watu wenye kipato kizuri na sio muhimu kwa ajili ya watoto wao kujikinga na ugonjwa wa corona.

Kehogo alisema licha dhana hiyo, wazazi wengi walilalamika kutokuwa na uwezo wa kununua barakoa baada ya kufungua shule kwa sababu kipindi cha likizo ya ugonjwa wa corona hakukuwa na shughuli za kiuchumi kama magulio na minada ili kuweza kuuza bidhaa zao.

Hata hivyo aliwataka wazazi kujitahidi kuwanunua watoto hata barakoa za kushona ambazo ni bei nafuu na wanaweza kuzimudu.

"Hatuwezi kuwaambia wanafunzi lazima waje na barakoa shuleni kwani wengi wao hawatokuja kwa singizio cha barakoa, hivyo tunatumia busara ya kuweka mkazo kwenye kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni," alisema Kehogo.

Mmoja wa wazazi Elizabeth Agustino, anayefanya kazi za usafi katika nyumba za kulala wageni katika kitongoji cha Kiomboi wilayani humo alisema kuwa ugonjwa wa corona ulileta changamoto kwa upande wake hasa kwenye kutafuta kipato chake na watoto wake wawili.

"Najua suala la kuvaa barakoa kwa wanafunzi shuleni na ni agizo la serikali. Mimi ni muathirika wa ugonjwa wa corona hasa kiuchumi niliterereka sana kutokana na kazi yangu ya kufanya usafi kwenye nyumba za wageni, hakukuwa na wageni kutoka nje ya wilaya hivyo nilikuwa nakaa tu nyumbani," alisema Agustino.

Regina Madaha mkazi wa Lulumba ambaye ni mama wa watoto watatu anayefanya shughuli za kuuza mboga na vitafunwa wilayani humo, alisema kuwa kutokana na kipato chake duni ameshindwa kuwanunulia watoto wake barakoa baada ya kufungua shule.

Madaha alisema kuwa amepata maelezo kutoka shuleni kwa watoto wake kuwa wanatakiwa kuwa na barakoa kama njia ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa corona, lakini tatizo la kiuchumi kutokana na ugonjwa corona hakuweza kuuza vitafunwa na kutembeza mboga.

Naye, Nicholus Kukwibwa, mfanyabiashara katika stendi kuu ya mabasi Kiomboi, alisema kipato chake ni kidogo kwa kuwa anahitaji pesa kwa ajili ya kuhudumia familia yake ikiwamo kununua barakoa za watoto, lakini kipato chake duni.

Kukwimba alisema, elimu ya uvaazi barakoa kwa watu wazima imepewa kipaumbele kuliko wanafunzi ambao wanahitaji kujikinga, lakini kipato duni hakiwezi kutosheleza kununua barakoa za familia nzima.

Fundi cherehani katika soko la Kiomboi, Fred Nasoro, alisema ushonaji wa barakoa tangu kufunguliwa shule umeshuka kwa kuwa wakati wa likizo wazazi wengi walijitokeza kushona barakoa.

Licha ya kushona barakoa za vitambaa, Nasoro pia anauza barakoa hizo kwa bei ya Sh. 1,000, lakini tangu shule zifunguliwe kwa muda wa wiki nzima hajauza barakoa hata moja.

Akizungumzia suala la wanafunzi kuvaa barakoa shuleni, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Linno Mwageni, alisema serikali inaendelea kutoa elimu ya kujikinga na corona hasa shuleni, lakini wazazi wengi wanachukulia suala hilo kama la mtu binafsi.

Mwageni alisema kuwa hata hivyo wazazi wanaangalia kupitia mikusanyiko mbalimbali ya serikali na kuona kuwa wengi hawavai barakoa na hivyo hawaoni umuhimu wa kuwapa watoto wao barakoa kama njia ya kujikinga na corona.

Aliongeza kuwa kwa sasa bei ya barakoa imeshuka za vitambaa zinauzwa Sh. 500, lakini wazazi hawaoni thamani na umuhimu wa kuwanunulia watoto wao.

twiga cement
HEIDELBERGCEMENT Group

UNAUDITED RESULTS
FOR THE SIX MONTHS ENDED 30 JUNE 2020

CHAIRMAN'S STATEMENT
Despite strong competition in the cement manufacturing industry and uncertainties brought about by COVID-19, Tanzania Portland Cement Public Limited Company (TPC PLC) delivered a strong operating result when compared to the year 2019. Turnover and sales volume increased by 7% and 8% respectively.

The operating performance of the plant and availability of the machinery was good, ensuring clinker production level higher than year 2019, all within an environment where the Health and Safety of our employees and contractors is paramount. The continued focus on delivering excellent customer service, the selling of high quality products, and the belief in maintaining strong customer relationships enabled TPC PLC to again demonstrate its strength as the leading player in the industry.

Prospects
The cement demand in Tanzania and in the East-African region has been growing steadily in recent years. TPC PLC is well placed to meet this growing demand and will continue to work to maintain its market leadership and position.

Appreciation
The Board would like to thank all its stakeholders for their support during this difficult period. We have every confidence that TPC PLC will continue to deliver value for the shareholders and community in the future.

BY ORDER OF THE BOARD

Hakan Gurdal
Chairman of the Board
15.07.2020

| INCOME STATEMENT | JAN - JUN 2020 TZS'000 | JAN - JUN 2019 TZS'000 |
|---|---|---|
| Revenue | 181,454,388 | 160,786,649 |
| Cost of sales | (113,688,511) | (101,222,624) |
| **Gross profit** | **67,765,877** | **59,564,025** |
| Other operating income | 2,278,447 | 557,566 |
| Selling and administrative expenses | (1,585,357) | (1,394,806) |
| Administrative expenses | (9,315,110) | (8,555,282) |
| Depreciation and amortisation | (8,626,083) | (9,786,410) |
| Other operating expenses | (1,467,018) | (1,689,277) |
| **Operating profit** | **49,050,756** | **38,695,816** |
| Financial items | 1,585,255 | (1,106,328) |
| **Profit before tax** | **50,636,011** | **37,589,488** |
| Taxes on income | (15,692,080) | (11,391,507) |
| **Profit for the year** | **34,943,931** | **26,197,981** |

| BALANCE SHEET | 2020 TZS'000 | 2019 TZS'000 |
|---|---|---|
| **ASSETS** | | |
| Intangible fixed assets | 823,264 | 875,361 |
| Tangible fixed assets | 131,529,045 | 136,874,862 |
| Other non-current assets | 10,358,0975 | 20,899,663 |
| **Non.current assets** | **142,710,406** | **158,649,886** |
| Inventories | 58,987,795 | 54,480,298 |
| Trade and other receivables | 56,934,604 | 49,019,785 |
| Cash and cash equivalents | 60,817,350 | 33,632,943 |
| **Current assets** | **176,739,749** | **137,133,026** |
| **TOTAL ASSETS** | **319,450,155** | **295,782,912** |
| **EQUITY & LIABILITIES** | | |
| **Equity** | **214,565,616** | **198,955,802** |
| Lease liabilities | 6,610,379 | 9,401,928 |
| Long term provisions | 8,070,602 | 8,604,351 |
| Provision for deferred taxes | 16,188,193 | 19,775,009 |
| **Non-current liabilities** | **30,869,174** | **37,781,288** |
| Lease liabilities | - | - |
| Current income tax payable | 1,568,115 | 932,772 |
| Trade and other payables | 69,100,427 | 54,500,366 |
| Dividend payable | 3,346,823 | 3,612,684 |
| **Current liabilities** | **74,015,365** | **59,045,822** |
| **TOTAL EQUITY & LIABILITIES** | **319,450,155** | **295,782,912** |

**Tanzania Portland Cement Public Limited Company**
**P.O.Box 1950**
**Dar-es-salaam**
**Tanzania**
**www.twigacement.com**
**Email: info@twigacement.com**

# TPB yanunulia shule kompyuta za mil. 15/-

**Na Neema Hussein,** RUVUMA

BENKI ya TPB Tanzania imetoa zaidi ya Sh. milioni 15 kununua kompyuta kwa ajili ya Shule ya Sekondari ya Wasichana Feo, wilaya ya Songea, mkoani Ruvuma ili kuwaongezea hamasa ya wanafunzi na walimu wa shule hiyo kufanya vizuri kitaaluma.

Mtendaji Mkuu wa Benki hiyo, Sabasaba Moshingi alisema, msaada huo ni sehemu ya kurudisha fadhila kwa jamii na ahadi aliyoitoa wakati wa mahafali ya kidato cha nne mwaka uliopita.

Alisema kwa kutambua juhudi kubwa zinazofanywa na Shule ya Sekondari ya Wasichana Feo, benki ya TPB imeona ipo haja ya kutoa sehemu ya faida yake katika kuchangia upatikanaji na utoaji wa elimu bora kwa wanafunzi na walimu wa shule hiyo.

Moshingi alisema, kompyuta hizo zinakwenda kuchochea hali ya kujisomea kwa wanafunzi wa shule hiyo pekee ya wasichana inayofanya vizuri kitaaluma katika mkoa huo na walimu kutumia kwa ajili ya kuandaa masomo na mitihani kwa wanafunzi.

Aliongeza mwaka 2019 TPB ilitenga kiasi cha fedha kila mwaka kwa ajili ya kusaidia huduma mbalimbali za kijamii na mwaka jana TPB ilitenga Sh. milioni 300 kati ya hizo milioni 15 zimetumika kununua kompyuta 10 kwa ajili ya shule hiyo.

Aliwataka Watanzania wakiwamo wafanyakazi wa Feo Sekondari kutumia benki za TPB ili kunufaika na huduma zake ikiwamo mikopo inayowalenga watu binafsi, wafanyabiashara wadogo, wa kati na kampuni.

Kwa upande wake Mkuu wa shule hiyo, Luciana Msabila, alisema shule hiyo ilianzishwa mwaka 2016 ikiwa na wanafunzi 78 kwa mikondo miwili ya A na B pamoja na walimu saba na sasa ina wanafunzi zaidi ya 300 na walimu 15.

Tangu ilipoanzishwa imefanya vizuri katika matokeo ya mitihani ya kidato cha pili kwa miaka mitatu mfululizo 2017, 2018 na 2019.

Alisema, katika matokeo ya mwaka jana ambayo ni ya kwanza kwa wanafunzi wa kidato cha nne tangu ilipoanzishwa, kati ya wanafunzi 62 waliofanya mtihani huo waliopata daraja la kwanza walikuwa (38), Daraja la pili (22) na Daraja la tatu (2) na hakuna aliyepata daraja la nne wala aliyefeli.

# DC aja juu wanaotia hofu mauaji ya wenye ualbino

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKUU wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, amesema anachukizwa na baadhi ya mashirika yanayofikia ofisini kwake kutambulisha miradi ya kupambana na mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi na wazee.

Hata hivyo, amesema anashangazwa na hatua hiyo kwa kuwa tangu awe mkuu wa wilaya hiyo, matukio hayo hayajawahi kuripotiwa.

Macha aliyabainisha hayo jana wakati wa kikao cha kutambulisha mradi wa kulinda na kutetea haki za wazee, hasa wanawake kutokana na vitendo vya kikatili na manyanyaso, utakaotekelezwa na Shirika la Kutetea wazee Shinyanga (TAWLAE) katika kata tisa na vijiji 36 Halmashauri ya Mji wa Kahama.

Alisema hivi karibuni lilifika moja ya shirika linalopambana na mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi ofisini kwake kutambulisha mradi wa kupambana na mauaji hayo, lakini alisema aliwafukuza ofisini kwa maelezo kuwa wanakwenda kuyaongezea hofu makundi hayo badala ya kuyasaidia na kuibua majonzi ya kwa wananchi.

Aidha, Macha alisema tangu amefikia wilayani hapa haijawahi kuripotiwa matukio ya mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi na wazee, lakini anashangaa kuona mashirika yanajitokeza kutambulisha miradi hiyo badala kusaidia mahitaji ya wenye ulemavu wa ngozi hasa mafuta na kofia za kujikinga na jua.

"Shirika litakalokuja kufanyakazi wilayani hapa lazima tufahamu yanakuja kufanya nini, yana malengo gani na elimu gani yanatoa kwa wananch," alieleza na kuongeza:

"Endapo tutabaini shirika linaendelea na shughuli zake mitaani bila kutambua hayo tutalichukulia hatua za kisheria. Wananchi wameshasahau vitendo hivyo halafu mashirika yanaanza kuibua majonzi."

Meneja mradi wa Help Age International, Joseph Mbasha, alisema mauaji ya vikogwe na watu wenye ulemavu wa ngozi kwa imani za kishirikina yamepungua kwa kiasi kikubwa, na mwaka 2023 shirika litahakikisha hakuna matukio ya mauaji yatakayoripotiwa tena.

Hata hivyo, alisema mwaka 2000/2015 matukio ya mauaji ya vitendo vya kikatilia kwa wazee na wenye ulemavu wa ngozi nchini nzima yalikuwa 700 hadi 500, huku mwaka 2016/17 vilikuwa 350 hadi 100 na mwaka 2018/19 vilikuwa 56 hadi 13.

Mwenyekiti wa Baraza la Wazee la Halmashauri ya Mji wa Kahama, Wilfred Birago, alipongeza Halmashauri hiyo kwa kuboresha afya za wazee kwa kuwakatia bima za afya za CHF ikiwamo kuwatengea chumba cha wazee na daktari wa kuwasikiliza matatizo yao.

Alisema mwaka wa fedha 2018/2019, Halmashauri ilitenga Sh. milioni 11.7 na kuwakatia bima za afya ya CHF zaidi ya wazee 3,380, hivyo kurahisisha huduma za afya kwa wazee.



Mhadhiri Msaidizi wa Chuo Kikuu Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Benard Adam (kushoto), akirudisha fomu za kuomba ridhaa ya kuteuliwa kugombea ubunge Jimbo la Kigamboni kwa Katibu wa Jumuiya ya Vijana CCM (UVCCM), Yusuph Mabena, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wahitimu SUA kuwainua vijana wa vijijini

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

USHIRIKA wa Wajasirimali Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUGECO), unakusudia kuwatumia vijana wa maeneo ya vijijini kuanzisha benki za uzalishaji wa mbegu za mazao ili kuongeza kasi ya upatikanaji wa mbegu bora kwa wakulima.

Hatua hiyo ya SUGECO ni moja ya utekelezaji wa mpango mkakati wa Serikali wa kujengea vijana uwezo wa kushiriki katika kilimo ili kuwa na uwakika wa ajira kwa lengo la kulisaidia kundi hilo kuondokana na umasikini kupitia sekta hiyo hasa katika kipindi hiki cha kuelekea uchumi wa viwanda.

Kauli hiyo imetolewa na Mwenyekiti wa Bodi ya SUGECO, Dk. Anna Temu, wakati wa hitimisho la mafunzo ya siku tano ya kilimo cha umwagiliaji wa matone, mboga na matunda pamoja kuongeza thamani mazao ya bustani kwa vijana 80 kutoka mikoa ya Songwe, Mbeya, Iringa, Njombe na Morogoro yaliyofadhiliwa na SUGECO pamoja na Shirika la HEIFER.

Dk, Temu, ambaye pia ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) alisema hatua hiyo imelenga kusaidia wakulima kuachana na matumizi ya mbegu za mazoea, ambazo kwa sasa hazina ufanisi badala yake watumie mbegu bora zinazoongeza tija pamoja na kukabiliana na magonjwa mbalimbali ili kuongeza kipato.

Mkurugenzi wa SUGECO, Revocatus Kimario, alisema mafunzo hayo yamelenga kuwabadilisha vijana hao kutoka kilimo cha mazoea na kufanya kilimo biashara kinachotegemea mahitaji ya soko kwa muda uliopo kwa kuzingatia elimu waliopewa na watalaamu wa kilimo bora.

Alisema yalihusisha zaidi elimu ya vitendo kwa asilimia 80 na nadharia kwa asilimia 20 ambapo pia wamejifunza namna ya kutumia teknolojia za kilimo cha mfumo wa umwagiliaji, mbinu bora za kilimo, elimu ya kujitambua na afya, elimu ya ujasiriamali na mbinu za uzalishaji wa mazao lishe.

Mmoja wa vijana hao, Hoffaman Mahenge kutoka Iringa, alisema wamejifunza kilimo biashara wanachoweza kulima kwa kuangalia mahitaji ya soko, huku wakidhibiti wadudu waharibifu kwa kutumia mimea mingine na sio kemikali kutoka viwandani kwa kuwa bidhaa zinazohitajika katika soko la hivi sasa hazitaji matumizi ya kemikali.

Akifunga mafunzo hayo, Mratibu wa Kitaifa wa Mkakati wa Vijana kushiriki katika kilimo kutoka Wizara ya Kilimo, Levilian Ngaiza, alisema lengo la Serikali ni kuhakikisha vijana wanatumia fursa mbalimbali za kilimo kujiajiri badala ya kusubiri ajira za serikali.

Alisema serikali imekaribisha wahisani mbalimbali kutoa fursa kwa vijana kutumia sekta ya kilimo, hivyo ni lazima kundi hilo kuzichangamkia pamoja na kueneza elimu hiyo kwa vijana wenzao waliopo katika maeneo ya vijijini nao waweze kuondokana na umasikini.

# TPSF yawavuta wawekezaji Italia sekta kilimo, biashara

Na Enock Charles

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), imewaalika wawekezaji kutoka nchini Italy kuja kuwekeza katika sekta mbalimbali za kiuchumi nchini zikiwemo sekta ya kilimo na biashara.

Akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kufanya mazungumzo na

Balozi wa Italia nchini, Roberto Mengoni mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa TPSF, Angelina Ngalula, alisema mazungumzo katika kikao chao waliangazia fursa zilizopo kwenye sekta ya kilimo na biashara,

"Kikao chetu na Balozi wa Italia kimekuwa kizuri kwani tumejadili fursa mbalimbali za kibiashara na uchumi zilizopoTanzania. Kikao chetu kililenga kuinufaisha sekta binafsi hasa kwenye sekta za kilimo na biashara," alisema Ngalula.

Aidha, Ngalula aliesema kupitia kikao hicho, Watanzania hasa wakulima na wafanyabiashara watanufaika zaidi kwani Balozi Mengoni ameahidi kutuunganisha na taasisi za kifedha za Italia ambazo zitawawezesha kupatikana kwa mikopo ya kuendesha shughuli za biashara.

Ngalula alisema kupitia kikao hiko, TPSF imewakaribisha wawekezaji kutoka Italia kuja kuwekeza kuwekeza pia majengo ya kuhifadhi mazao kwenye bandari na viwanja vya ndege kipindi yanaposubiri kusafirishwa nje ya nchi.

Alimwomba Balozi kuwasaidia kupata masoko kwenye viwanda Italia ili wakulima waweze kupata fursa ya kuuza mazao yao ya matunda na mbogamboga kwenye viwanda hivyo moja kwa moja.

Alishukuru Tanzania kupata nafasi ya kushiriki kwenye maonyesho ya mbogamboga Septemba mwaka huu, lakini kutokana na janga corona, maonnyesha hayo yatafanyika kwa njia ya mtandao kutoka nchini Italia na kutoa fursa kwa wakulima kuonyesha mazao yao ya mbogamboga yanayolimwa nchini.

Balozi Mengoni aliishukuru TPSF kwa mwaliko na kuahidi kushirikiana na taasisi hiyo kutangaza fursa zilizopo Tanzania kwenye sekta ya kilimo na biashara kwa wafanyabiashara wa Italia.

"Naomba niwahakikishie kuwa nafasi yangu kuzitangaza fursa zilipo hapa kwa nchi yangu ili Waitaliano waje kwa wingi kuwekeza Tanzania,"alisema Mengoni na kupongeza ushirikiano uliopo baina ya nchi hizo mbili.

Naye kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TPSF, Zacky Mbenna, alisema kikao

hiko kililenga kuangazia fursa za kibiashara zilizopo kwenye nchi hizo mbili kwa sekta binafsi ya Tanzania na Italia .

"Wenzetu Italia sekta binafsi imepiga hatua kubwa hivyo kwa kushirikiana nao tutapata nafasi ya kujifunza namna wao wanavyoendesha sekta hii ambayo mchango wake ni mkubwa kwenye soko la ajira, "alisema Mbenna.




Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Turiani wakipeleka madawati darasani baada ya makabidhiano. Benki ya NMB imekabidhi misaada ikiwamo mabati, vitanda na mashine za kunawia mikono kwa Shule za msingi Kisauke, Mzimuni, Osyterbay, Msasani 'B', Tandale Magharibi, Turiani sekondari pamoja na kituo cha afya cha Mabwepande. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Miradi ya Kigamboni yampa DC matumaini ya uwekezaji

Na Frank Monyo

MKUU wa Wilaya ya Kigamboni, Sarah Msafiri, amesema kukamilika mradi mkubwa wa umeme sambamba na mchakato wa kufunga mfumo wa gesi wilayani humo kutachochea uwekezaji na uzalishaji katika viwanda na kuongeza pato la taifa.

Alibainisha hayo mwishoni mwa wiki wilayani humo alipotembelea Kiwanda cha Lake Ciment kinachozalisha saruji ya nyati katika hafla fupi ya kuwapongeza wafanyakazi waliofanya vizuri katika uzalishaji pamoja na kupokea tasmini ya uzalishaji katika kipindi cha ugonjwa wa corona.

Alisema kuwa serikali imetoa Sh. bilioni 26 kwa ajili ya mradi mkubwa wa umeme katika eneo la Dege ambao unatarajiwa kukamilika Agosti mwaka huu ili kuongeza uzalishaji katika kiwanda hicho.

"Nataka kuwahakikishia kuwa, mradi wa umeme utakapokamilika tutawaletea megawati tano ili kuongeza uzalishaji zaidi... najua mnajua tumeanza mchakato wa kuleta gesi katika maeneo haya ya viwanda kwani serikali imepima 'Block' 400 za viwanda hivyo kiwanda cha Lake Ciment kitakuwa wanufaika wa kwanza," alisema Msafiri.

Alisema kiwanda hicho kimekuwa kikilipa kodi ya Sh. bilioni 30 kwa mwaka, hivyo ni kiwanda ambacho kinachochea ukuaji wa uchumi kwa kiasi kikubwa.

Alisema saruji inayozalishwa katika kiwanda hicho imekuwa ikitumika katika miradi mikubwa ya serikali kama mradi wa uzalishaji wa umeme Rufiji, ujenzi wa reli ya kisasa, ujenzi wa madaraja makubwa na ujezi wa barabara za juu Ubungo.

Msafiri ameupongeza uongozi wa kiwanda hicho kwa kuendelea na uzalishaji na hawakupunguza wafanyakazi katika kipindi cha mlipuko wa corona.

Aliwataka vijana ambao wameajiriwa katika kiwanda hicho kutoshiriki katika kuvu-

## Shule, kituo cha afya Kinondoni zasaidiwa

Na Elizabeth Zaya

SHULE za Msingi tano, sekondari moja na kituo cha afya kimoja zilizopo wilayani Kinondoni, mkoani Dar es Salaam, vimekabidhiwa vifaa vyote vikiwa na thamani ya jumla ya Sh. milioni 36.

Vifaa hivyo vimetolewa na Benki ya NMB na kupokelewa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Daniel Chongolo.

Vifaa vilivyokabidhiwa kwa nyakati tofauti jana ni mabati 180, madawati 200, vifaa vya kutakasia mikono (mashine) sita, viti na meza 100, vilivyotolewa kwa Shule za Msingi Oysterbay, Msasani, Tandale Magharibi, Mzimuni na Kisauke na Sekondari ya Turiani.

Pia, vitanda na magodoro kwa Kituo cha Afya cha Mabwepande, ambako hafla ya kukabidhi vifaa vya shule ilifanyika Shule ya Sekondari Turiani, Magomeni na kuhudhuriwa na Chongolo, pamoja na Ofisa Elimu Msingi Manispaa ya Kinondoni, Kiduma Mageni.

Kaimu Meneja wa Kanda wa NMB, Seka Urio, alisema changamoto za sekta ya elimu na afya ni miongoni mwa vipaumbele vya NMB, na kuwa inatambua juhudi za serikali katika kusimamia sekta hizo kwa nguvu zote kwa kutoa elimu bure na kuboresha utoaji wa huduma hizo mjini na vijijini.

"Ingawa Serikali inafanya makubwa, sisi kama wadau tuna wajibu wa kuunga mkono juhudi hizi za maendeleo kwa kusaidia jamii, kwani kupitia jamii hii hii ndio imeifanya benki ya NMB kuwa hapa ilipo na kubwa kuliko benki yoyote hapa nchini," alisema Urio.

Alieleza NMB ilipopata maombi ya kusaidia walifarijika na kuamua mara moja kushirikiana na Serikali kupitia uongozi wa shule husika, ili kuwa chachu ya maendeleo ya elimu kwa jamii hasa katika Shule hizi za msingi zikiwemo Kisauke, Msasani B, Oysterbay, Mzimuni, Tandale Magharibi, Turiani Sekondari na Kituo cha Afya Mwabepande.

"Kwa maana hiyo, NMB tumeamua kushirikiana na shule hizo, ambazo kila shule inapata madawati 50 na viti vyake. Pia tumechangia Shule ya Msingi Mzimuni mabati 150, huku Shule tano zikipata mashine za kunawia mikono na maji tiririka ilikuzuia maambukizi ya Covid-19," alisema na kuongeza:

"Pia tumechangia vitanda na magodoro kwa kituo cha afya cha Mabwepande. Misaada yote ikiwa na thamani ya Sh. milioni 36 kwa ujumla."

Kwa upande wake, Chongolo aliipongeza NMB kwa moyo wa kuijali na kuithamini jamii, na kwamba misaada mbalimbali inayotoa katika sekta za afya na elimu, inaacha alama njema katika mioyo ya wanafunzi, walimu na jamii kwa ujumla ,na kuwa inasaidia harakati za Serikali katika kuboresha miundombinu na kutatua changamoto.

# Wakulima walia kutimuliwa maeneo yao

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

BAADHI ya wakulima wa korosho, ufuta na mahindi wa Kitongoji cha Nakanami kijiji cha Mkwapa katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara wamepinga agizo la serikali ya kijiji cha Mkwapa linalowataka kuhama maeneo yao wanayolima mazao hayo kwa madai maeneo hayo ni hifadhi ya akiba.

Wakizungumza wakiwa kwenye maeneo ya mashamba yao, wakulima hao walisema serikali ya kijiji ya chao kwa kushirikiana na uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi umewapa notisi ya kuwataka kuyahama maeneo hayo ambayo wamekuwa wakiendesha shughuli zao za kilimo.

Wakulima hao walisema serikali ya kijiji imewataka ifikapo Agosti wawe wameshaondoka na kusitisha shughuli zote za kilimo kwenye maeneo hayo kwa madai kuwa maeneo hayo hayapaswi kufanya shughuli zozote za kilimo kwa sababu serikali ya kijiji iliyatenga kwa ajili ya hifadhi ya akiba kwa serikali ya kijiji.

Rashidi Mande alisema alianza kulima kwenye mashamba hayo mazao mbalimbali ikiwamo ufuta, mahindi na korosho tangu mwaka 2013, lakini wanashangazwa hivi sasa kuelezwa na serikali ya kijiji chao kuwa wanatakiwa kuyahama maeneo hayo, hivyo wanaiomba serikali ya kijiji hicho kutengua agizo hilo.

Alisema wakulima wamekuwa wakilima kwenye mashamba hayo kwa miaka mingi sasa na hata mazao yao yanatambuliwa na serikali ya kijiji, na wamekuwa wakishiriki katika kutoa michango mbalimbali ya maendeleo.

Lucia Hokororo, alisema fedha wanazopata kwenye mashamba yao wamekuwa wakizitumia katika kuwasomesha watoto wao, hivyo kitendo cha wao kuelezwa kuhama kwenye mashamba hayo ni kutaka maisha yao yawe magumu. Mwenyekiti wa serikali ya Kijiji cha Mkwapa, Oscar Mlowola, alithibitisha kutoa agizo mapema mwaka huu kwa wakulima hao kuyahama maeneo hayo kwa sababu wanalima maeneo hayo yalitengwa na serikali kama hifadhi ya akiba na serikali ya kijiji cha Mkwapa.

Alisema serikali ya kijiji inaendelea kusimamia agizo lake la kutaka wakulima hao kuhama mara moja kwa vile uamuzi huo ulifanyika katika mkutano mkuu wa kijiji, hivyo lazima yatekelezwe kwa vitendo. "Hawa wakulima ambao wanalima kwenye maeneo hayo sio wakazi wa kijiji chetu bali wametoka nje ya kijiji chetu na kuvamia kwenye maeneo haya na kuanza shughuli za kilimo bila kupitia katika serikali ya kijiji kupata utaratibu...lazima waondoke tu," alisema Mlowola.



Robot aitwaye Pepper ambaye alikuwa kivutio kikubwa katika banda la Vodacom kwenye Maonyesho yaliyomalizika ya 44 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (Sabasaba) akijibu maswali mbalimbali aliyoulizwa na wateja waliotembelea banda hilo. Vodacom iliibuka mshindi wa kwanza katika kipengele cha Mawasiliano na Tehama. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jela miaka 2 kwa kutukana matusi ya nguoni

**Na Hellen Mwango**

MKAZI wa Zanzibar Mbuyu, Daurat Salum Suleiman, amehukumiwa kulipa faini ya Sh. milioni tano au kwenda jela miaka miwili kwa kosa la kumtukana mama yake mkubwa (matusi ya nguoni), kupitia mtandao wa kijamii wa Instagram.

Hukumu hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Martha Mpaze.

Alisema mahakama yake bila kuacha shaka upande wa Jamhuri umethibitisha kosa dhidi ya mshtakiwa la kudhalilisha mzazi wake kupitia mtandao wa kijamii.

"Mahakama hii baada ya kusikiliza ushahidi wa mashahidi sita wa upande wa Jamhuri ukiwamo mchunguzi, umethibitisha kosa bila kuacha shaka dhidi ya mshtakiwa ni kweli alimtukana Sabaha Said Chondoma, maarufu kama Teacher, inamtia hatiani kwa kosa hilo" alisema.

Alisema baada ya kusikiliza mashahidi alibaini maneno aliyoandika mshtakiwa yalikuwa na lengo la kumdhalilisha mlalamikaji (Chondoma), licha ya kwamba Suleiman alikana kutenda kosa hilo wakati anajitetea.

"Baada ya kupitia ushahidi wa mashahidi sita na vielelezo, mshtakiwa amepatikana na hatia ya kumdhalilisha kimtandao Chondoma, atalipa faini ya Sh. milioni tano na akishindwa kulipa fedha hiyo atakwenda jela kutumikia kifungo cha miaka miwili," alisema Hakimu Mpaze.

Kabla ya hukumu hiyo, hakimu aliauliza upande wa Jamhuri kama wana chochote cha kusema, mawakili wa Serikali Gloria Mwenda na Grace Mwanga, walidai kuwa hawana rekodi za nyuma za mshtakiwa na pia ni kosa lake la kwanza, lakini aliomba adhabu kali ili iwe fundisho kwa wengine.

Wakili wa mshtakiwa huyo, Nassoro Hamis, aliomba mahakama hiyo impatie mshtakiwa adhabu ya faini (adhabu ndogo), kama alivyosema Wakili wa Serikali kuwa ndiyo kosa lake la kwanza.

Wakili Hamis alidai kuwa anaomba adhabu hiyo kwa mambo mawili, jambo la kwanza mshtakiwa ni mgonjwa na suala la pili Suleiman ana watoto watano na wote ni wadogo wa mwisho yupo chini ya mwaka mmoja, familia kama hiyo inahitaji mtu wa kuwahudumia ambaye ni mama.

Ilidaiwa kuwa Desemba 28 na 29, 2018 ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mshtakiwa alitumia lugha ya kumdhalilisha Chondoma kwa kutumia mfumo wa kompyuta unaoitwa Instagram kwa nia ya kumnyanyasa kwa kuposti maneno ya matusi.

Mshtakiwa alikuwa anachati na mtoto wa Chondoma Instagram (Sharifa Ally), lakini baadaye mshtakiwa alianza kuposti matusi akimtukana mama yake Sharifa ambaye ndiye mlalamikaji katika kesi hiyo.

# DC: Watendaji msisubiri ziara za viongozi kutatua kero

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MKUU wa Wilaya ya Morogoro, Bakari Msulwa, amewataka watendaji kutatua kero za wananchi kwa wakati badala ya kuendelea kusubiri ziara za viongozi.

Alitoa agizo hilo wakati wa mkutano wake wa kusikiliza na kutatua kero za wananchi uliofanyika kwenye viwanja vya Shule ya Msingi Kiwanja cha Ndege , Manispaa ya Morogoro.

Alisema dhamira ya Serikali ya awamu ya tano ni kuona inatatua kero za wananchi, na kwamba suala la utatuzi wa kero hizo halitakiwi kuendelea kusubiri ziara za viongozi, badala yake zitatuliwe kwenye ngazi zinazohusika na zitatuliwe kwa wakati.

Mkuu wa wilaya, alisema kuwa migogoro mingi na kero nyingi zinasababishwa na kutowajibika kwa baadhi ya watendaji ambao wamepewa dhamana ya kuwaongoza wananchi kwa ajili ya kuwaletea maendeleo.

Msulwa alisema suala la kutotatua kero za wananchi katika ngazi ya Serikali za Mitaa ni kinyume cha dhamira ya Serikali ya kuwatumikia wananchi wote bila ubaguzi ambalo pia ni kinyume cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Sheilla Lukuba, aliwataka watendaji wa kata, na mitaa kuitisha mikutano ya kisheria katika maeneo yao na kusoma taarifa za mapato na matumizi ya miradi ya maendeleo katika maeneo yao.

" Niwatake viongozi na watendaji wa mitaa na Kata ndani ya halmashauri yatu jengeni utamaduni wa kuwatembelea wananchi na kusikiliza kero na changamoto zinazowakabili ikiwa ni pamoja na kuzitafutia ufumbuzi" alisema Lukuba.

Nipashe
Spotika




10-BORA USAJILI WENYE MAFANIKIO MSIMU HUU UK. 12&13




# TIMU 5 ZILIZOZAWADIWA PENALTI NYINGI ULAYA 2019 -20

Cristiano Ronaldo akiifungia Juve moja ya penalti kati ya 12 alizopiga na kufunga msimu huu. **PICHA: MTANDAO**

## ISIKUPITE

PIERRE-EMERICK Aubameyang, amekuwa mchezaji wa nne Arsenal kufunga mabao mawili kwenye mechi ya kimashindano katika Uwanja wa Wembley, baada ya Reg Lewis (1950 fainali Kombe la FA), Charlie Nicholas (1987 fainali Kombe la Ligi) na Alexis Sanchez (2015 nusu fainali Kombe la FA).




**ROME,** Italia

PENALTI imekuwa ni uamuzi unaozua utata sana kwenye mchezo wa soka duniani.

Penalti inatolewa na mwamuzi kwa timu pinzani kama mchezaji wake amemzuia kufunga wakati akiwa kwenye nafasi nzuri ya kufanya hivyo ndani ya eneo la hatari. Pia inatolewa kama mlinzi au mchezaji anapounawa mpira ndani ya eneo la hatari langoni mwake.

Lakini penalti zimekuwa zikizua utata mwingi, kwani wengi huwa wanaona kama wameonewa kwa kupewa adhabu hiyo.

Makala haya yanaangalia timu tano katika ligi kubwa tano za Ulaya zilizozawadiwa penalti nyingi zaidi msimu huu, hadi sasa...

### #1: LAZIO - 15

Lazio ndio timu inayoongoza kwa kupewa penalti nyingi zaidi katika ligi kubwa tano za Ulaya, katika Ligi Kuu ya Italia, Serie A. Lakini wao wanaonekana kuwa na bahati zaidi.

Lazio imepewa penalti 15 msimu huu, ndio nyingi zaidi kwa Ulaya. Huku mechi chache zikiwa zimebaki kumalizika kwa msimu hu, idadi hiyo inaweza kuongezeka.

Ciro Immobile ndiye amekuwa mpigaji wa penalti wa Lazio msimu huu, akipiga 12 na kufunga 11 kati ya hizo. Immobile, Joaquin Correa na Caicedo wamezawadiwa penalti nyingi zaidi kwa Lazio, wote wakipata tatu kila mmoja.

Zaidi ni kwamba, mafanikio ya Immobile kufunga penalti 31 kwenye Serie A ni mengi zaidi kuliko mchezaji yeyote baada ya Francesco Totti mwenye 36.

### #2: GENOA - 14

Tofauti na Lazio, ambao wamenufaika zaidi kwa penalti, Genoa inayoshika nafasi ya 18 ambao wanaweza kushuka daraja kutoka Serie A, hawajawa na bahati licha ya kupata penalti hizo.

Genoa ilikosa penalti nne kati ya 14 walizozawadiwa msimu huu. Mabao yao yaliyotokana na penalti ni robo ya jumla ya mabao yote msimu huu.

Winga wa kushoto wa Genoa, Domenico Criscito ndiye mpigaji penalti wa kikosi hicho, akifunga saba kati ya tisa msimu huu. Stefano Sturaro amefunga mara mbili kwa Genoa.

### #3: LECCE NA MANCHESTER UNITED - 13

Lecce ni timu ya tatu kutoka Serie A iliyopata penalti nyingi zaidi kati ya ligi kubwa tano Ulaya msimu huu.

Wakiwa nafasi ya 17 kwenye msimamo, Lecce imefunga penalti 10 kati ya 13 walizozipata msimu huu wa 2019-20. Kama ilivyo kwa Genoa, Lecce pia robo ya mabao yake yametokana na penalti.

Marco Mancosu amefunga penalti nyingi zaidi kwa Lecce msimu huu, akifunga nane kati ya tisa. Straika Khouma Babacar ndiye alizawadiwa penalti nyingi zaidi kwa kufanyiwa faulo eneo la hatari.

Miamba wa Ligi Kuu ya England, Manchester United wamezawadiwa penalti 13 msimu huu, ikiwa ndiyo timu iliyovuna nyingi zaidi kwa EPL.

Hata hivyo, nyingi wamepoteza, kwani wamekosa nne kati ya penalti hizo. Marcus Rashford amefunga sita kati ya nane, huku Bruno Fernandes akifunga zote tatu alizopiga. Wote Paul Pogba na Anthony Martial wamekosa penalti moja kila mmoja. Rashford ndiye amezawadiwa penalti nyingi zaidi msimu huu, akiwa mchezaji aliyezawadiwa zaidi ndani ya kikosi cha Manchester United kwa msimu huu wa 2019-20 wa Ligi Kuu.

### #4: JUVENTUS - 12

Miamba hao wa Serie A, Juventus wamekuwa na wakati mzuri kwa msimu huu wa 2019-20 kwenye Serie A.

Straika wake, Cristiano Ronaldo amefunga penalti zote 12 alizopiga kwa Bianconeri hao msimu huu. Nahodha huyo wa Ureno alifunga pia dhidi ya Atalanta wakati mchezo huo ukimalizika kwa sare ya kufungana mabao 2-2.

### #5: VILLARREAL - 11

Timu pekee kutoka Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, kuwapo kwenye orodha hii ni Villarreal ambao wamefunga 10 kati ya 11 walizozawadiwa msimu huu.

Santi Cazorla anaongoza kwa kuwa na rekodi, akifunga zote kati ya nane alizopiga. Winger Moi Gomez ameshinda tatu, huku Samu Chukuweze na Gerard Moreno wakipata mbili kila mmoja.

# 10-BORA USAJILI WENYE MAFANIKIO MSIMU HUU




HAALAND

**LONDON,** England

USAJILI wa wachezaji ni biashara isiyo na uhakika wa mafanikio. Si tu suala la kipaji, lakini kuna mambo mengi ambayo yanaweza kufanya usajili wa mchezaji kuwa na mafanikio kwa klabu au la.

**Huku fedha nyingi zikiwa zinatumika kwenye mchezo huo siku hizi, ni rahisi kufanya makosa katika uhamisho wake. Skauti ya uhakika inatakiwa ili kupata mchezaji ambaye atafiti kwenye mahitaji.**

Hapa tunaangali 10-bora ya usajili uliokuwa na mafanikio chanya kwa timu zao msimu huu...

### #10. AARON WAN-BISSAKA | MANCHESTER UNITED

Uamuzi ya Manchester United kulipa pauni milioni 45 kwa Crystal Palace kwa Aaron Wan-Bissaka yaliibua minong'ono. Wan-Bissaka alifurahia msimu akiwa pale Palace hapo kabla. Hivyo, maswali yaliibuka kwamba huenda United imelipa fedha kwa mchezaji ambaye pengine alinga'ra kwa msimu mmoja tu.

Mmoja wa walinzi bora kwenye Ligi Kuu ya England, Wan-Bissaka ameweza kuhimili vizuri safu ya ulinzi wa kulia ya United. Uwezo wake wa kukaba ni kitu kizuri, na si mawinga wengi waliweza kumshinda wakiwa moja dhidi ya mmoja. Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 22 ameimarika na kuwa na uwezo mzuri mno wa kukaba na ni mlinzi wa kulia aliyekamilika.

Ingawa bado hajaichezea timu ya Taifa ya England, haina shaka yoyote ni suala la muda tu kuitwa kwenye kikosi hicho kinachonolewa na kocha, Gareth Southgate. Msimu huu, amecheza mechi 38 katika mashindano yote kwa 'Mashetani Wekundu' hao akitoa pasi za mwisho nne.

### #9. ERLING HAALAND | BORUSSIA DORTMUND

Moja ya usajili bora msimu huu. Erling Braut Haaland alijiunga na Borussia Dortmund Januari mwaka huu kutoka Red Bull Salzburg kwa ada ya pauni milioni 17. Mchezaji huyu mwenye kipaji cha aina yake tayari ameonyesha thamani yake kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, akifunga mara kwa mara kwa miamba hao.

Akiwa amekataa uhamisho wa kwenda Manchester United, uamuzi wa Haaland kwenda Ujerumani unaonekana kama ulikuwa na mafanikio makubwa zaidi kwake. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, amefunga mabao 16 katika mechi 18 alizocheza pale Dortmund.

Raia huyo wa Norway msimu huu umekuwa mwenye mafanikio kwake. Kwa pande zote mbili Dortmund na Salzburg amecheza jumla ya mechi 40 katika mashindano yote, akifunga mara 44 na kutoa pasi za mwisho tatu.

### #8 BRUNO FERNANDES | MANCHESTER UNITED

Bruno Fernandes aliwasili pale Manchester akitokea Sporting Lisbon Januari kwa ada ya pauni milioni 47 na tayari ameonyesha umuhimu wake kwa klabu hiyo.

Kiungo huyo amekuwa nguzo muhimu zaidi tangu ajiunge na klabu hiyo, kwani alichukua muda mfupi sana kuizoea ligi hiyo. Fernandes ameonyesha kiwango cha kuvutia zaidi kwa kikosi cha United. Kiungo mbunifu, anayejiamini na ambaye 'ameifufua' timu kuwa na mtazamo tofauti kabisa.

Mechi 10 za ligi alizoichezea klabu hiyo, raia huyo wa Ureno amefunga mabao saba na kutoa pasi za mwisho sita.

Upatina wake na Paul Pogba kwenye safu ya kiungo umekuwa na manufaa makubwa zaidi, na wengi wanatarajia kwamba mengi zaidi yanakuja kutoka kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. Wengi wamekuwa wakimlinganisha na Eric Cantona.

### #7. MATTHIJS DE LIGT | JUVENTUS

Matthijs de Ligt alikataa uhamisho wa kwenda Paris Saint-Germain, Manchester United na Barcelona ili asajiliwe kule Juventus kipindi cha majira ya joto. Miamba hao wa Italia waliilipa Ajax pauni milioni 67.5 kwa ajili ya kupata saini yake, na kumfanya kuwa mmoja wa walinzi ghali zaidi duniani.

Mlinzi huyo wa kati alianza taratibu maisha pale Juventus. Hata hivyo, de Ligt sasa anaonekana kuwa kwenye kiwango chake, na moja ya jina la kwanza kwenye kikosi cha kwanza cha kocha Maurizio Sarri. Beki huyo mwenye umri wa miaka 20, ametengeneza upatina mzuri zaidi na mkongwe Leonardo Bonucci.

De Ligt amecheza mechi 33 katika mashindano yote kwa Juventus msimu huu, akifunga mabao matatu. Anaongoza kwa kuokoa hatari nyingi kwa klabu hiyo.

### #6. MAURO ICARDI | PARIS SAINT-GERMAIN

Mauro Icardi aliamua kumaliza mahusiano yake ya utata kule Inter Milan kwa kwenda kujiunga na Paris Saint-Germain, awali akitua kwa mkopo. Miamba hao wa Ufaransa wakalipa pauni milioni 45 Mei mwaka huu ili kumsajili moja kwa moja.

Rekodi ya ufungaji mabao ya Icardi inazungumza yenyewe. Raia huyo wa Argentina amefunga mabao 124 katika mechi 219 alizoichezea Inter Milan, pia alikuwa nahodha kwa muda mfupi. Hata hivyo, nje ya uwanja amekuwa mtata.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, amechukua mikoba ya Edinson Cavani kwenye safu ya ushambuliaji ya PSG, akiiongoza vizuri. Katika mechi 31 kwa klabu hiyo, mchezaji huyo wa zamani wa Sampdoria amefunga mabao 20 na kutoa pasi za mwisho mbili.

### #5. ROMELU LUKAKU | INTER MILAN

Romelu Lukaku ndiye mtu aliyerithi mikoba ya Mauro Icardi pale Inter Milan. Na amekuwa na kiwango cha kuvutia sana kwa miamba hao wa Italia ni rahisi kusema kwamba, Icardi pengo lake halijaonekana.

Raia huyo wa Ubelgiji alijiunga na Inter Milan akitokea Manchester United kwa ada ya pauni milioni 74. Amekuwa mfungaji nguzo wa klabu hiyo na mfumo wa kocha, Antonio Conte umemfiti zaidi.

Conte alimtaka wakati akiwa kule Chelsea, lakini Lukaku aliamua kwenda kwa 'Mashetani Wekundu' kwa wakati ule. Sasa wameungana, na matokeo yake yameonekana. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, amecheza mechi 41 kwa klabu hiyo katika mashindano yote, akifunga mabao 26 na kutoa pasi za mwisho tano.

### #4. FERLAND MENDY | REAL MADRID

Real Madrid wanajaribu kuziba pengo la gwiji Marcelo kwa muda sasa. Wakawapa nafasi wahitimu wa akademi ya vijana, Achraf Hakimi na Sergi Reguilon, ambao wameshindwa kuonyesha viwango vyao kwa nafasi ya mlinzi wa kushoto kwa klabu hiyo.

Los Blancos hao waliamua kutumia kiasi cha pauni milioni 43 kumleta Ferland Mendy kutoka Lyon. Mendy ameonyesha kiwango cha kuvutia kwa safu ya ulinzi ya kushoto pale Real Madrid msimu huu.

Raia huyo wa Ufaransa amekuwa akibadilishana vizuri na Marcelo msimu huu. Katika mechi 28 alizocheza kwenye mashindano yote klabuni hapo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, ametoa pasi za mwisho mbili.

### #3. WISSAN BEN YEDDER | AS MONACO

Mmoja wa wachezaji anayechukuliwa poa sana duniani, Wissam Ben Yedderh amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia msimu huu.

Ben Yedder alijiunga na Monaco akitokea Sevilla kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 35, huku Rony Lopes akienda Sevilla ikiwa sehemu ya usajili huo. Raia huyo wa Ufaransa amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia sana kwa miamba hao wa Ligue 1, akiwa kileleni mwa wanaongoza kufunga mabao katika ligi pamoja na Kylian Mbappe.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Toulouse mwenye umri wa miaka 29, awali alikuwa akihusishwa na mpango wa kwenda Manchester United kabla ya kuhamia Monaco na hadi sasa amecheza mechi 31 katika mashindano yote, akifunga mabao 19 na kutoa pasi za mwisho nne.

### #2. CHRISTOPHER NKUNKU | RB LEIPZIG

Paris Saint-Germain bila shaka yoyote imekuwa na wahitimu wazuri kutoka kwenye akademi yao, lakini inaonekana kuzinufaisha zaidi klabu nyingine tofauti na miamba hao wa Ufaransa.

Christopher Nkunku ni mmoja wa wachezaji hao. Alihamia RB Leipzig kutoka PSG kwa ada ya pauni milioni 12, na amekuwa mmoja wa wanaotengeneza mabao kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, msimu huu.

Mchezaji huyu wa timu ya Taifa ya Ufaransa chini ya umri wa miaka 21, amekuwa akicheza mara kwa mara kwa kikosi hicho cha kocha, Julian Nagelsmann, akicheza katika sehemu tofauti tofauti. Amekuwa akicheza kama winga, kiungo wa kati, mshambuliaji pamoja na winga wa kushoto kwa kikosi hicho cha Ujerumani msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, amecheza mechi 42 katika mashindano yote kwa klabu hiyo, akifunga matano na kutoa pasi za mwisho 13.

### #1. BENJMIN PAVARD | BAYERN MUNICH

Benjamin Pavard alijiunga na Bayern Munich kutoka Stuttgart kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 31. Dili hili lilikubaliwa Januari mwaka 2019, huku Pavard akijiunga na klabu hiyo kipindi cha majira ya joto.

Amekuwa na kiwango cha kuvutia kwenye safu ya ulinzi ya Bayern. Kutokana na majeraha ya mlinzi wa kati, Lucas Hernandez na Niklas Sule kwa kipindi kirefu cha msimu huu, Mfaransa huyo amecheza mechi nyingi zaidi kwa Bavaria hao.

Akiwa na uwezo wa kucheza nafasi ya beki wa kulia pamoja na mlinzi wa kati, nyota huyo wa zamani wa Lille amekuwa mtu muhimu kwa kikosi cha Hansi Flick. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, amecheza mechi 48 katika mashindano yote kwa klabu hiyo, akifunga mabao manne na kutoa pasi za mwisho sita.

## Nukuu

"Xavi atakuwa kocha wa Barca karibuni au baadaye, lakini kwa sasa hatutafuti kocha tupo na Quique [Setien]," **Rais wa Barcelona , Josep Maria Bartomeu.**



"Hapana, hapana. Sihisi hivyo. Najihisi tu ni mtu mwenye bahati kuwa hapa na wachezaji kila siku. Kuwa na klabu, ndilo jambo ninaloliona kuwa na bahati na ndio maana nafurahia hilo kila siku. Kwa sababu siku moja hali hiyo itamalizika, kama ambavyo ilishawahi kutokea," **Kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane, akisisitiza yeye si "special one" baada ya kuibebesha timu hiyo ubingwa wa LaLiga.**



"Kwa sasa fahari yetu kwa Barca, tunatakiwa kuelekeza akili yetu kwenye kombe ambalo tunaweza kulipigania, ambalo ni Ligi ya Mabingwa Ulaya, kwenye Ligi [Ligi Kuu] unatakiwa kujiangalia wewe mwenyewe – tuliliachia litukimbie wenyewe," **Mshambuliaji wa Barca, Luis Suarez**






Kiungo mshambuliaji wa Simba, Claotus Chama, akijaribu kuwalamba chenga mabeki wa Yanga, pamoja na kipa wake Mechata Mnata, kwenye mechi ya robo fainali ya Kombe la FA kwenye Uwanja wa Taifa Simba, ikishinda 4-1 Julai 12, mwaka huu. **PICHA: MAKTABA**

# SIMBA ILIVYOZIKOSESHA YANGA, AZAM KIMATAIFA

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara ya kwanza baada ya miaka mingi, timu za Azam na Yanga hazitoiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa kwa pamoja, kutokana na kukosa nafasi ya uwakilishi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho.

**Kwa miaka mingi sasa, Simba, Yanga na Azam zimekuwa mbili kati ya hizo zikiwakilisha nchi kwenye michuano hiyo, tangu Azam ilipoanza kucheza Ligi Kuu msimu wa 2008/09 na moja kati ya timu hizo ndiyo inakosa nafasi hizo.**

Msimu ujao utashuhudiwa timu za Yanga na Azam zikiwa nje ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho na Simba pekee kati hizo tatu ndiye atakayeiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa.

Sababu kubwa kwa Yanga na Azam kukosa michuano ya kimataifa msimu ujao ni timu ya Simba.

Simba imetwaa ubingwa wa Tanzania Bara kama misimu miwili iliyopita, lakini safari hii haijatolewa kwenye hatua za awali kama misimu iliyopita ilivyotolewa dhidi ya Green Warrios na Mashujaa kwenye Kombe la FA, badala yake imekomaa mwanzo mwisho.

Hii ilikuwa ndiyo fursa pekee kwa timu za Yanga na Azam mmoja wapo kupata walau nafasi ya kuwakilisha kimataifa. Badala yake zote mbili msimu huu zimekosa. Kwa sababu gani? Ni kwamba timu hizo zimepitia njia ngumu. Njia yenye msitu mnene wenye simba mkali.

Tofauti na timu ya Namungo FC ambayo imepata bahati ya mtende kwa kupata tiketi ya kucheza michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika kabla hata ya kucheza fainali ambayo itapigwa kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga mkoani Rukwa kati yake na Simba.

Namungo kwa upande wake imepita njia nyepesi ambayo haikuwa na vikwazo vingi. Njia ya lami, mjini na pia kuna taa.

Huenda hata Yanga na Azam zingepita njia iliyopitia Namungo, moja wapo saa hizi nayo iko fainali.

Tatizo timu hizo zote zimekutana na Simba. Zimetolewa na Simba. Azam ilianza kupata mkosi baada ya Kagera Sugar kufungwa mabao 2-1 dhidi ya Yanga.

Kilichotokea ni kwamba Simba iliuchukulia mchezo wake dhidi ya Azam kwa uzito mkubwa kwa sababu tu ya kwenda kulipa kisasi kwa Yanga. Huenda ingekuwa vinginevyo kama Kagera Sugar ingeshinda. Ukweli ukabaki pale pale kuwa Azam ilipita njia au anga ngumu za simba.

Yanga nayo baada ya kuifunga Simba bao 1-0 kwenye mechi ya mzunguko wa pili ilikuwa ni kama imejichongea. Simba ilionekana kuwa kutafuta nafasi hiyo adhimu kwa ajili ya kulipiza kisasi na si kushiriki michuano ya Kombe la Shirikisho kwa sababu tayari tiketi ya Ligi ya Mabingwa ilikuwa nayo. Yanga nayo ikawa ni kama imeingia kwenye mtego ule ule wa kupita njia ya simba aliyekuwa amejeruhiwa, anayesubiri kulipa kisasi.

Hivi ndivyo Yanga na Azam zilipojichanganya na kupita njia yenye simba...

**AZAM 0-2 SIMBA**

Azam ambayo msimu ujao michuano ya kimataifa itayasikia kwenye 'bomba', ilianza safari yake ya Kombe la FA kwenye raundi ya tatu kwa kucheza dhidi ya African Lyon na kupata ushindi wa mabao 4-1 kwa mikwaju ya penalti, baada ya kutoka sare ya bao 1-1 kwa dakika zote 90.

Baada ya hapo ilitinga raundi ya nne na kucheza dhidi ya Friends Ranger ya Manzese. Kwenye mechi hiyo ilitoa kipigo kizito cha mabao 6-0 dhidi ya Friends Ranger na kufanikiwa kutinga raundi ya tano ambapo ilikutana na Ihefu ya Mbeya.

Kwenye mechi hiyo, timu zote zilitoka sare ya bila kufungana, lakini Azam ilishinda kwa mikwaju 5-4 ya penalti na kufanikiwa kufika robo fainali ya michuano hiyo. Shughuli pevu kwao ilikuwa ni kwenye hatua hiyo, kwani ilikutana na Simba na kupata kipigo cha mabao 2-0, ikawa ndiyo mwisho wao wa safari ya kwenda kucheza mechi ya kimataifa, kombe la Shirikisho Afrika.

**YANGA 1- 4 SIMBA**

Yanga, baada ya kukosa ubingwa, nguvu yao ilihamishia kwenye michuano hii. Kwa bahati mbaya sana ilipitia njia ambayo ina Simba.


Yanga ilianza michuano hiyo kwa kuitungia Iringa United kwa mabao 4-0, baada ya hapo ikapangwa kucheza dhidi ya Prisons na kwenye mechi hiyo, Yanga ilishinda mabao 2-0.

Baada ya hapo, ikapata nafasi ya kucheza na timu iliyokuwa Daraja la Kwanza Tanzania Bara, lakini kwa sasa imepanda Ligi Kuu, Gwambina FC.

Kwenye mechi hiyo Yanga ilishinda bao 1-0 na kukata tiketi ya kwenda kucheza mechi ya robo fainali dhidi ya Kagera Sugar. Ni mechi ambayo Yanga ilishinda mabao 2-1 na moja kwa moja ikapata nafasi ya kucheza dhidi ya Simba.

Ni mechi ambayo ilikuwa chungu kwa Yanga, ilipokosa nafasi ya uwakilishi wa michuano ya kimataifa kwa kuchapwa mabao 4-1.

## JE, WAJUA?




KIPIGO cha mabao 2-0, Arsenal ilichokitoa kwa Manchester City juzi, kinaifanya kuweka rekodi ya kutinga fainali ya Kombe la FA mara 21, huku ikiwa inaongoza kuutwaa ubingwa huo zaidi kwa kuubeba mara 13. Kadhalika, Asenal imewatoa mabingwa watetezi wa Kombe la FA katika mara zote sita ilizokutana nao.



**HABARI DODOMA**

# DC aeleza sababu kutotia nia ubunge

**Na Mwandishi Wetu,** CHEMBA

MKUU wa Wilaya ya Kilolo, Mkoani Iringa, Asia Abdallah, amesema ameshindwa kutia nia ya kugombea ubunge wa Viti Maalum Mkoa wa Dodoma kutokana na kuhitaji kuendelea kumsaidia Rais John Magufuli, katika wilaya hiyo.

Kauli hiyo aliitoa mwishoni mwa wiki katika Maulidi iliyofanyika katika Kijiji cha Magadi, wilayani Chemba, ikiwa ni siku mbili baada ya kuhitimishwa kwa uchukuaji na urejeshaji wa fomu kwa watia nia wa ubunge, udiwani na uwakilishi kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM). Alisema alikuwa na mpango wa kutia nia hiyo, lakini ameshindwa kutokana na kutii maneno ya rais kwa kuwa bado anamuhitaji kuendelea kumsaidia kwenye majukumu ambayo atahitaji amsaidie.

"Katika vitabu vya dini mnatambua tumeelekezwa kutii mamlaka, hivyo nimetii mamlaka ya uteuzi wangu, mimi ni nani mpaka niwe na kiburi mbele ya kiongozi wangu nisitii mamlaka," alisema.

Akizungumza na waumini wa dini ya Kiislamu katika Maulidi hayo, Mkuu huyo alisema hatua kali zitaendelea kuchukuliwa kwa wazazi wasiopeleka shule watoto ili wilaya iendelee kupata kizazi chenye wasomi.

"Hakuna kisingizio chochote cha kutokumpeleka mtoto shule kwa kuwa serikali imeondoa vikwazo vyote ikiwamo ada na michango mingine na serikali kila mwezi inatumia zaidi ya Sh. bilioni 23 kwa ajili ya watoto wetu wapate elimu bila malipo, zamani sisi tulikuwa tunasoma tunajilipia ada," alisema Abdallah.

Aliwataka viongozi wa dini wa wilaya hizo kuwahamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi kwenda kupiga kura kuchagua viongozi watakaowaletea maendeleo chanya akiwamo Rais Magufuli.

Alisema katika historia Chemba na Kondoa kuna tatizo la watu kutokujitokeza kwenda kupiga kura wakati ni haki yao ya kimsingi kikatiba.

Naye, Mwalimu wa Madrasa, Aisha Mohamed, aliwataka wazazi kuwalea watoto wao katika maadili mema ili kuwa na kizazi chenye utii siku za mbeleni.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, akiwaonyesha waandishi wa habari (hawapo pichani), masanduku mawili yenye ujazo wa kilogramu 35 yanayosadikiwa kuwa na dawa za kulevya aina ya bangi yaliyokamatwa katika Kijiji cha Mbande, wilaya ya Kongwa yakisafirishwa kutoka Dodoma kwenda Tanga, jana
**PICHA: PETER MKWAVILA**

# Maduka pembejeo yafungwa kukiuka uendeshaji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BARAZA la Veterinari nchini limeyafunga baadhi ya maduka ya wafanyabiashara wa pembejeo za kilimo na mifugo jijini Dodoma, baada ya kubaini ukiukwaji wa uendeshaji wa maduka hayo.

Maduka hayo yalifungwa jana baada ya kubainika upungufu kadhaa ikiwamo kuendeshwa na watu wasio na taaluma.

Akizungumza katika ukaguzi huo, Msajili wa Baraza hilo, Dk. Bedan Masuruli, alisema baraza hilo lililazimika kuchukua hatua ya kufunga baadhi ya maduka kutokana na kukiuka kanuni na sheria za utoaji huduma.

Alisema huduma za dawa zinatakiwa kutolewa na wataalam ambao ndio watatoa dawa sahihi na inayokidhi viwango vya kumsaidia mfugaji.

"Wataalam wote wa afya ya wanyama wanatakiwa kuhuwisha majina yao katika daftari la usajili, katika operesheni hii Baraza pia linahakikisha huduma zinazotolewa zinakidhi viwango utoaji wa dawa sahihi, na chanjo iuzwe kwa bei elekezi iliyotolewa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi," alisema.

Nao, baadhi ya wafanyabiashara ambao hawajafungiwa maduka yao, walishauri wenzao kuhakikisha wanazingatia sheria na taratibu zilizowekwa na serikali ili kutoa huduma bora.

# Mkandarasi apewa siku 14 kukamilisha nyumba za RC, DC

**Na Augusta Njoji,** CHAMWINO

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, ametoa siku 14 kwa mkandarasi wa mradi wa ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa Wilaya ya Dodoma na ukarabati wa nyumba ya Mkuu wa mkoa huo kukamilika ili viongozi hao wahamie kwenye makazi yao.

Agizo hilo alilitoa jana jijini hapa akiwa katika ziara yake ya kikazi ya kukagua maendeleo ya ujenzi huo ambao unasimamiwa na Ofisi ya Katibu Tawala wa mkoa huo kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Alisema ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa wilaya hiyo umeanza muda mrefu na fedha zimeshatolewa tangu mwaka 2018 na ujenzi umeanza mwaka 2019, lakini hadi sasa bado haujakamilika.

"Nimekagua karibu mara tatu na nimeagiza yale yale na muda wa mwisho walioahidi kukamilisha ni Mei 7, mwaka huu, lakini miezi miwili sasa imeisha bila kukamilisha, kwasababu kazi zilizobaki ni kidogo nimeelekeza zikamilike ndani ya siku 14, walitaka muda zaidi, lakini nimekataa, walishapewa fedha zote, walitakiwa wajaze nguvu kazi ili kukamilisha na kumpokea Mkuu wa wilaya anayekuja, nitaongea na Mkuu wa Kikosi wa Suma JKT ili kufanyia kazi haraka," alisema.

Kuhusu ukarabati wa nyumba ya Mkuu wa mkoa, Dk. Mahenge alisema anaishi kwenye nyumba ya Jeshi la Magereza kutokana na aliyopaswa kuishi kufanyiwa ukarabati na kuwataka kukamilisha haraka kwa kuwa Kamishna wa jeshi hilo anahitaji nyumba hiyo.

"Hapa wananiambia ukarabati utakamilika hadi Agosti 15, mwaka huu, nimekataa nimewapa siku 14 tu, wakamilishe. Nilichobaini katika ziara yangu ni kasi isiyoendana na muda kwenye utekelezaji wa miradi hii, na inatokana na nguvu kazi ndogo," alisema. Alisema nyumba hiyo kiasi cha Sh. milioni 300 kimetolewa kwa ajili ya ukarabati mkandarasi alipaswa kujipanga kukamilisha kwa muda uliopangwa kwa mujibu wa mkataba.

"Mkandarasi aliyopewa ni wa Wizara ya Ujenzi alipaswa kufanya kwa muda uliopangwa, fedha aliyopewa si kidogo," alisema.

Akizungumzia ujenzi wa nyumba ya Katibu Tawala wa Wilaya ya Chamwino, alisema "ujenzi wa nyumba yake ni matokeo ya kubana matumizi nyumba ya Mkuu wa Wilaya ya Dodoma na Katibu Tawala wa Wilaya ya Chemba na kiwango kilichobaki tukaamua kujenga nyumba hiyo nimekagua, lakini nimebaini kasi ya ujenzi ipo chini, nimeagiza waongeze kasi ili jengo likamilike na Katibu Tawala aanze kuishi."

Aliwataka makandarasi ambao wamepewa fedha kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi hiyo na kuacha kutumia nguvu kazi ndogo hali inayochelewesha miradi.

Katika Hospitali ya Uhuru, Dk. Mahenge alisema ujenzi wake una gharimu Sh. bilioni 3.9 na tayari zaidi ya Sh. bilioni tatu zimelipwa.

"Kwenye hospitali ya Uhuru ujenzi unaenda vizuri tatizo ni muda, wanatakiwa kukamilisha Agosti 23, mwaka huu, tumesema wakamilishe haraka hospitali ianze kufanya kazi," alisema.





## Halmashauri Nyanda za Juu Kusini zaagizwa michango ya Nanenane

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI zote za mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, zimeagizwa kuhakikisha zinakamilisha michango ya ushiriki wa sherehe za Maonyesho ya wakulima (Nanenane) katika Kanda hiyo kabla ya kesho saa 10 jioni.

Wakuu wa mikoa ambayo bado halmashauri zake hazijawasilisha michango, wameagizwa kusimamia.

Agizo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo, ambaye alikuwa mwenyekiti wa Kikao cha pili cha maandalizi wa maonyesho hayo katika Ukumbi wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwenye viwanja wa John Mwakangale jijini Mbeya.

Alitoa agizo hilo baada ya Sekretarieti ya maandalizi ya maonyesho hayo kuzitaja baadhi ya Halmashauri na Sekretarieti za mikoa kuwa hazijakamilisha michango hiyo huku zingine zikidaiwa michango hata ya miaka iliyopita.

Alisema michango hiyo inatakiwa iwasilishwe mapema ili kuiwezesha Sekretarieti ya maandalizi kufanya maandalizi haraka na kufanikisha sherehe hizo.

"Kila Mkuu wa Mkoa anatakiwa kusimamia michango hii ili tufanikishe maonyesho haya ambayo ni muhimu sana, kuna Halmashauri hapa zimetajwa kuwa zinadaiwa michango hata ya mwaka 2018, kila Mkurugenzi atekeleze wajibu wake," alisema Wangabo.

Mkuu Mkoa wa Iringa, Ally Happi, aliwataka maofisa kilimo wa mikoa yote kuhakikisha wanawafundisha wakulima kuhusu kilimo bora na kuhakikisha teknolojia zitakazoonekana kwenye maonyesho hayo ziwafikie hata ambao hawatahudhuria.

Alisema kilimo ni sekta muhimu kwenye maendeleo ya taifa na mkulima moja mmoja hivyo ni vema wananchi wakawezeshwa kuzalisha kisasa ili kuongeza tija.

Aliwataka maofisa kilimo na sekretarieti za mikoa kuzingatia taratibu katika kuwashindanisha wakulima kwenye maeneo yao ili kuwapata wawakilishi sahihi watakaoshiriki kwenye Kanda.

"Mkichagua wawakilishi kwa upendeleo ni lazima mkifika kwenye Kanda mtashindwa, lakini mkizingatia vigezo vya uzalishaji bora ni lazima mtafanikiwa kuwapata washindi ambao watawawakilisha vyema," alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mussa Homera, alisema baadhi ya maofisa kilimo huwa wanapokea rushwa kutoka kwa baadhi ya Halmashauri ili wazitangaze kuwa ndizo zimeshinda kwenye maonyesho.

Aliwataka viongozi hao kuacha tabia hiyo mara moja ili washindi watakaopatikana wawe halali na waweze kuziwakilisha vyema Halmashauri zao.

# Ma-RC watoboa siri kutogombea ubunge

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wakuu wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, waliokuwa na nia ya kuacha nafasi zao na kwenda kugombea ubunge kwenye majimbo, wameeleza sababu zilizowafanya waachane na mipango hiyo na kusalia kwenye nafasi zao.

Wakizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha maadalizi ya sherehe za maonyesho ya wakulima (Nanenane) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, jijini Mbeya, walisema moja ya sababu za kuahirisha kugombea ni kuridhika na nafasi walizoteuliwa kuzitumikia.

Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo, alisema aliamua kuridhika na nafasi yake baada ya maelezo ya Rais John Magufuli ya kuwataka waridhike na nafasi zao na wasiwe na tamaa kama walivyofanya wengine.

Alisema yeye alikuwa anatamani kwenda kugombea ubunge katika Jimbo la Mlele mkoani Rukwa, lakini baada ya kutafakari niliamua kuachana na tamaa hiyo na kuendelea na wadhifa wake.

"Mwaka 2015, niligombea udiwani kwenye Kata ya Lembeni katika wilaya ya Mwanga mkoani Kilimanjaro na nikashinda, nafasi hiyo niliitumikia kwa miezi nane pekee, nikateuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Nanyumbu mkoani Mtwara, na nafasi hiyo niliitumikia kwa mwaka mmoja na miezi nane nikateuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Rukwa," alisema na kuongeza:

"Sasa baada ya kutafakari tamaa yangu ya kwenda kugombea ubunge, niliamua kuacha na kuridhika na nafasi yangu, hivyo nawashauri wateule wenzangu tuache tama, maana mwenye mamlaka na nafasi yako ni yule aliyekuteua na ukiondoka unamwachia ampe mwingine."

Naye Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mussa Homera, alisema pia alikuwa na mipango ya kwenda kugombea, lakini baada ya kauli ya Rais Magufuli ya kuwatahadharisha wateule wake, aliamua kuachana na nia yake hiyo.

Alisema wananchi wa Jimbo lake (ambalo hakulitaja), walikuwa wanamuhitaji, lakini kutokana na kauli ya rais aliamua kuachana na matamanio hayo ya wananchi na kuamua kusalia kwenye nafasi yake aliyoteuliwa kuitumikia.

Homera alisema ni vema wateule wa rais wakaendelea kuwatumikia wananchi wa maeneo yao, na kwamba uchapakazi wao utaonekana na wanaweza wakateuliwa kwenye nafasi kubwa zaidi ya zile wanazozitumikia kwa sasa.

"Aliyetuteua ana imani na sisi kuwa tunafaa kumsaidia kuwatumikia wananchi kwenye maeneo yetu, sasa mimi nilipopima kina cha maji niliamua kuacha kugombea licha ya wananchi kunihitaji, tuendelee kufanya kazi kwa bidii," alisema Homera.

Hivi karibuni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alitangaza kupitia vyombo vya habari kuhusu kuahirisha nia ya kwenda kugombea ubunge katika Jimbo la Iringa Mjini kwa kuheshimu maelekezo ya Rais Magufuli ambaye ndiye mteule wake na kubaki kusimamia miradi ya maendeleo.

Kauli hiyo aliirudia akiwa Ikulu ya Chamwino jijini Dodoma alipopewa nafasi ya kutoa neno alipopewa nafasi hiyo wakati rais Magufuli alipokuwa anawaapisha baadhi ya viongozi aliowateua wakiwamo wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya, wakurugenzi na makatibu tawala.

Alisema Serikali imepeleka miradi mingi mkoani Mbeya, hivyo anatakiwa kusimamia ili itekelezwe kwa ufanisi.



Baadhi ya vijana wanaofanya kazi ya kuchimba mchanga kandokando ya mto, wakiupakia kwenye lori juzi, shughuli ambayo wamezuiwa kuifanya kutokana na uharibifu wa mazingira. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Wanahabari Mbeya wapata viongozi wapya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA cha Wanahabari Mkoa wa Mbeya (MBPC), kimepata viongozi wapya ambao wanatarajiwa kukiongoza chama hicho kwa muda wa miaka mitano kuanzia 2020 mpaka 2025.

Viongozi hao walichaguliwa mwishoni mwa wiki wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka ambao ulisimamiwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi huo, Ezekiel Kamanga, Katibu wake, Esther Macha na Mratibu wa Chama hicho, Yonathan Kosam.

Kamanga alimtangaza Festo Sikagonamo, kuwa mshindi wa nafasi ya uenyekiti kwa kupata kura 11 akiwashinda Joseph Mwaisango na Fredy Jackson.

Aidha, aliwatangaza, Joseph Mwaisango kuwa Makamu Mwenyekiti Fredy Jackson. Kenny Mwakandyali (Katibu Mkuu) na Lukia Chasanika (Mtunza Hazina).

"Nawashukuru wanachama wote mlioshiriki kwenye zoezi hili, uchaguzi ulikuwa huru na wa haki na nawashukuru kwa kuweka imani kwa wanachama wenzetu hawa ili watuongoze kwa miaka mitano, ninachowaomba ni kuwapa ushirikiano ili tuvuke salama," alisema Kamanga.

Vilevile alisema wajumbe wa Mkutano huo waliwachagua Grace Mwakalinga, Elizabeth Nyivambe na Bosco Nyambege kuwa wajumbe wa Kamati Kuu kwa miaka mitano ijayo.

Pia alisema wanachama waliwachagua Fredy Jackson, kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mafunzo, Gabriel Mbwile kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi na Miradi na Ezekiel Kamanga kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya nidhamu.

Akizungumza kwa niaba ya viongozi waliochaguliwa, Sikagonamo aliwashukuru wanachama kwa kuendelea kumuamini.

Alisema atahakikisha anashirikiana na wananchama pamoja na viongozi wengine kuhakikisha chama kinapata maendeleo na wanachama wanufaika na uwanachama wao pamoja na kuendelea kushawishi wanahabari wengine kujiunga.

"Nawashukuru sana kwa kutuamini na kutuchagua kuwa viongozi wenu, hiki chama ni cha kwetu sote na ni wajibu wetu kuhakikisha tunashirikiana kukijenga, tunaomba mtupe ushirikiano ili tufanikishe jambo hili," alisema Sikagonamo.

Awali Katiba ya MBPC viongozi waliokuwa wanachaguliwa walikuwa wanatakiwa kukitumikia chama hicho kwa miaka mitatu, lakini baada ya Umoja wa Klabu za wandishi wa Habari nchini (UTPC) kuagiza mabadiliko, vyama wanachama kufanya uchaguzi kila baada ya miaka mitano.



# Ndege za kimataifa zaanza kutua Z'bar kwa kishindo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WATALII na abiria kutoka mataifa mbalimbali ni miongoni mwa wasafiri 80 waliotua juzi katika kiwanja cha kimataifa cha Abeid Amani Karume Zanzibar (AAKIA).

Abiria 80 hao waliingia Zanzibar na Shirika la Ndege la Qatar Air na ndege ya Dreamliner A 787, wakiingia visiwani humo baada ya kupungua kwa ugonjwa wa COVID-19 na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kufungua rasmi safari za anga.

Abiria hao walitua saa 2:30 juzi wakifuata taratibu zote za tahadhari za kiafya zilizowekwa uwanjani humo.

Akizungumza na wanahabari, Ofisa Uhusiano wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA), Mulhati Yussuf Said, alisema, kiwanja kimeanza kupokea ndege kutoka mashirika mbalimbali.

Alisema shirika hilo lilisitisha safiri za anga tangu Aprili 9 mwaka huu baada ya kuibuka kwa ugonjwa wa COVID -19 ulioyakumba mataifa mbalimbali na baadhi ya safari za anga zimeanza rasmi.

Said alisema kuwasili kwake ndege hiyo, kumeonyesha dalili nzuri kuwa sasa ugonjwa huo unaendelea kupungua na kumekuwapo kwa hali ya kuridhika kiafya juu ya janga la corona.

Alisema mashirika mengi yanaendelea kufanya mawasiliano na kiwanja hicho ili kuanzisha safari za anga na safari.

Hivyo, aliwataka Watanzania walioko nje na ndani ya nchi kueneza ujumbe kuwa kiwanja cha AAKIA kipo salama na wanaendelea kupokea abiria bila ya wasiwasi.

Ofisa Uhamiaji Mfawidhi katika kituo cha uhamiaji wa AAKIA, Bakari Mohamed Ameir, alisema wamekuwa na utaratibu bora kwa wageni wanaoingia katika kiwanja hicho huku wakizingatia usalama zaidi kujiepusha na maradhi.

Ameir aliwataka wageni kuendelea kutembelea mtandao wa Uhamiaji kwa ajili ya kuangalia utaratibu wa kuomba kibali cha kuingia nchini na kuondokana na usumbufu.



Amos Malima, Mkazi wa Kijiji cha Vilabwa wilayani Kisarawe mkoani Pwani, akijaza mafuta ya petroli kwa ajili ya kuyauza rejareja kwa waendesha pikipiki maarufu 'Bodaboda' katika mazingira yasiyo salama. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ataka mabadiliko uongozi wa shehia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Kaskazini 'B', Unguja Rajab Ali Rajab, amewataka masheha kupitia upya kamati walizozianzisha ili kuimarisha uwajibikaji miongoni mwa wajumbe wake.

Alisema kuna baadhi ya shehia kumekuwapo na tatizo la ushiriki mdogo wa wanakamati zinapotokea ziara ama shughuli za kijamii hali ambayo inaleta usumbufu kwa serikali inapofanya ufatiliaji wa huduma za kijamii

Akizungumza jana katika kikao cha pamoja na masheha hao ofisini kwake Mahonda, Rajab alisema lengo la kuundwa kwa kamati mbalimbali katika shehia ni kuwarahisishia wananchi kupata huduma muhimu kwa wakati sahihi pamoja na kuusaidia uongozi wa shehiya katika majukumu yake ya kila siku

Aliwataka masheha hao kusimamia utaratibu uliowekwa na serikali kwa kuhakikisha rasilimali hasa ardhi na na maeneo ya mabondeni hayavamiwi na wananchi na kutumiwa kinyume na utaratibu

Kwa upande wao masheha hao walisema kuna tatizo la uelewa kuhusu umuhimu wa kupata vibali vya ujenzi hali ambayo inaleta usumbufu mamlaka husika inapositisha shughuli za ujenzi kwa wananchi.

Waliiomba ofisi ya mamlaka ya maji wilayani humo kutatua tatizo la kukosekana huduma hiyo kwa wananchi ili kila mmoja aweze kulipia maji hayo bila ya vikwazo.

# Asisitiza kujali zaidi amani kuelekea uchaguzi Oktoba

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MCHUNGAJI Kiongozi wa Makanisa ya Kipentekoste Zanzibar (PEFA), Daniel Kwilemba Kwiyeya, amesisitiza umuhimu wa Watanzania kulinda zaidi amani wakati huu wa kuelekea kwenye uchaguzi mkuu.

Aliitaka jamii kusimamia na kudumisha amani na utulivu katika kipindi hiki na pia kuchagua viongozi watakaowafaa na si wasindikizaji.

Alitoa ushauri huo jana katika hafla ya kuzinduwa jengo la kanisa hilo liliopo Kisauni, Unguja.

Alisema kuwa katika kipindi cha uchaguzi hujitokeza mambo mengi ambayo mengine husababisha kutokea kwa vurugu.

Alieleza kuwa kipindi hiki jamii inatakiwa kuwa makini na isiruhusu matakwa yao yawatawale ili kuepusha migogoro itakayopelekea kuvunjika amani.

Kuhusu kanisa, alisema mbali na kufanya ibada pia limejengwa na litakuwa likihusisha shughuli mbali mbali za kijamii na kuiomba jamii kujitokeza kulitumia.

Aidha, alisema kuwa katika eneo hilo la kanisa kuna shule ambayo inafundisha madili ya Kizanzibari.

Ujenzi wa kanisa hilo unatarajiwa kutumia milioni 100 hadi kukamilika kwake na hadi sasa zimetumia shilingi milioni 48.

# Serikali yatoa bil. 20/- kulipa madeni ya korosho

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema Serikali imetoa Sh. bilioni 20 za kulipa madeni ya wakulima, wasafirishaji, wapuliziaji dawa na waendesha maghala ya korosho.

"Rais Magufuli ametoa fedha hizi kwa ajili ya Tandahimba, Masasi, Mtwara na Kibiti kwa ajili ya waliokuwa wamelipwa nusu, waliolipwa kiasi na wasiolipwa kabisa. Fedha hizi zitaanza kulipwa kesho asubuhi," alisema.

Alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na wanachama wa Chama cha Msingi (AMCOS) cha Matogoro na wakazi wa Tandahimba mkoani Mtwara, alikoenda kuhamasisha maandalizi ya msimu wa ununuzi wa korosho.

Alisema uhakiki uliofanywa kwa wakulima wa Kibiti, Rufiji, Mkuranga, Ruangwa, Liwale, Lindi, Tunduru na wilaya zote za mkoa wa Mtwara ulibaini kuwa wakulima na watoa huduma wote walikuwa wakidai zaidi ya Sh. bilioni 23.

"Katika hao, Tandahimba wanadai zaidi ya Sh. bilioni 9, Masasi wanadai Sh. bilioni 2.3 na Mtwara Vijijini wanadai Sh. milioni 884. Nyingine ni za Pwani na Lindi," alifafanua.

Waziri Mkuu alisema fedha hizo zimetokana na mfumo uliotengenezwa na wanunuzi ili kumnyonya mkulima katika msimu wa 2018/2019 kwa kununua kilo ya korosho kwa Sh. 1,500 badala ya Sh. 3,000 hali iliyolazimu Serikali kuingilia kati na kuamua kuzinunua korosho zote.

Waziri Mkuu alishuhudia Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Kilimo (TABD), Japhet Justine, akimkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, hundi ya Sh. 9,050, 846,030 ambaye pia aliikabidhi kwa viongozi wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Tandahimba na Newala (TANECU) na AMCOS ya Matogoro.

Awali, Mwenyekiti wa CCM mkoa wa Mtwara, Yusuph Nanila, alimuomba Waziri Mkuu atoe majibu ya lini wakulima wa Tandahimba watalipwa fedha zao, ambazo zimefikia zaidi ya Sh. bilioni 9.

Wakati huohuo, Waziri Mkuu amevitaka Vyama Vikuu vya Ushirika na AMCOS waweke kipaumbele cha kununua mashine ndogo ndogo za kubangulia korosho ili waache mtindo wa kuuza korosho ghafi.

"Ukibangua kilo tatu za korosho yenye maganda, unapata kilo moja ya korosho zilizobanguliwa. Kilo moja ya korosho yenye maganda inauzwa Sh. 2,400 kwa hiyo kilo tatu ni Sh.7,200, lakini ukizibangua, kilo moja inauzwa Sh.25,000. Ninawasihi tuanzishe viwanda vidogo vya kubangua korosho ili tupate fedha zaidi kwenye vyama vya msingi."



Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Sarah Msafiri, akipanda mti wa kumbukumbu katika Kiwanda cha Lake Cement kinachozalisha Saruji ya Nyati mwishoni mwa wiki, alipotembelea Kiwanda hicho Kigamboni jijini Dar es Salaam. Habari Uk. 9. **PICHA: FRANK MONYO**

# Ndikilo ahamasisha lishe bora Pwani

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Evarist Ndikilo, amewataka wakuu wa wilaya za mkoa huo kusimamia kikamilifu suala la lishe bora katika wilaya zao.

Ndikilo alitoa rai hiyo wakati akifungua kikao cha pili cha tathmini ya mkataba wa lishe kwa kipindi cha Januari-Juni, 2020, kilichofanyika Julai 16, mjini Kibaha.

Aliwataka viongozi hao wa wilaya kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu lishe bora na itakayoambatana na kuhamasiha watoto kupewa chakula wakiwa shuleni.

"Ndugu wajumbe tumeona tatizo la udumavu kitaifa ni asilimia 31 na sisi katika mkoa wetu tuna asilimia 23 kutokana na hali hii wakuu wa wilaya kwa kushirikiana na wataalamu wa afya tunatakiwa kusisitiza lishe bora kila mmoja katika eneo lake," alisema Ndikilo.

Alisema baada ya agizo hilo anatarajia kupata matokeo chanya kwa kila mmoja kusimamia katika eneo lake na kuhakikisha asilimia hiyo inapungua pamoja na kuondoa idadi ya watoto wenye udumavu inapungua.

Alitoa wito kwa wazazi wenye watoto shuleni kuwachangia chakula ili waweze kuepuka tatizo la udumavu kwa kukosa chakula.

Alipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga kwa kuvuka malengo ya kiwango kilichowekwa cha viashiria vya mkataba wa lishe na kuzitaka halmashauri nyingine za mkoa huo kuiga mfano wa halmashauri hiyo.

# W'biashara wanolewa kurahisisha mikopo

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mkuu wa Benki ya Letshego, amewataka wafanyabiashara wadogo nchini kuacha kufanya biashara kimazoea, badala yake wahuishe matakwa ya kitaaluma ili wajiweke kwenye mazingira mazuri kukopeshwa.

Andrew Tarimo alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam alipozungumza kwenye semina iliyoshirikisha wafanyabiashara wanaohudumiwa na benki hiyo.

Alisema kuwa, kama wafanyabiashara hao wakijenga utamaduni wa kutunza kumbukumbu za mauzo ya bidhaa zao pamoja na kufunga hesabu zao kila wamalizapo biashara, watakuwa kwenye mfumo rasmi wa ufanyabiashara na hivyo kuwa na uhakika wa kukopesheka.

Aliwataka kutambua kuwa muda wa kufanya biashara kimazoea umeisha, hivyo wajikite katika ufanyabiashara wenye tija, ili wachangie pato la taifa na kuiwezesha nchi kusonga mbele zaidi.

Mkurugenzi Mkuu huyo alisema kwa kutambua nafasi za wafanyabiashara wadogo katika kukuza uchumi wa nchi, benki hiyo imewawekea mazingira bora ya kukopeshwa, ikianza kwa kuwaondolea adhabu ya kushindwa kurejesha mkopo.

Alisema kuwa hata wakati ambao nchi ilikuwa kwenye janga la corona, benki hiyo ilisitisha urejeshwaji wa mikopo ya wajasiriamali kwa muda wa miezi mitatu, hivyo kuwapatia unafuu zaidi wa kibiashara.

"Semina hii na wafanyabiashara hawa tunawaelekeza masuala mbalimbali kuhusiana na biashara, lakini pia tunapata mrejesho kutoka kwao kuhusiana na nini wanataka benki yetu iwasaidie, hivyo sote tunasikilizana na kubadilishana mawazo," alisema.

Mkurugenzi Mkuu huyo aliongeza kuwa kwa sasa biashara zimeanza kurejea kama kawaida baada ya ugonjwa huo kupungua, na benki hiyo imeona ni vema kukutana na baadhi ya wafanyabiashara hao kujadiliana kuhusiana na nini kifanyike, ili kuboresha zaidi huduma za kibenki.

Mwenyekiti wa Bodi ya benki hiyo, Simon Jengo, alibainisha kuwa kama wafanyabiashara hao wakijituma zaidi kwenye biashara zao, watanufaika zaidi na hatua ya nchi kuingia uchumi wa kati.

"Wafanyabiashara mnatakiwa kujua mbinu za kufanya biashara ili ziwawezeshe kuendeleza biashara zenu zaidi ili kuchangia pato la taifa, mkinufaika nyie na siye kama benki ndiyo tutasonga mbele zaidi," alisema.

Semina hiyo ilihudhuriwa na wamiliki wa shule, vituo vya mafuta, wafanyabiashara wadogo, wa kati na wakubwa ambao pia walitoa maoni yao kuhusiana na nini wanataka benki ifanye kwao ili wakuze biashara zao.

HABARI KIMATAIFA

# 600,000 wafariki kwa corona duniani

**WASHINGTON,** Marekani

IDADI ya vifo kutokana na janga la virusi vya corona ulimwenguni imefikia watu 600,000, hali inayoashiria namna ulimwengu uko mbali na matumaini ya kurejea katika hali ya kawaida.

Shirika la Afya Duniani (WHO) limerekodi takribani maambukizi mapya 260,000 ya virusi vya corona. Hiyo ni rekodi mpya ya idadi ya juu zaidi ya ugonjwa huo kurekodiwa ulimwenguni kote ndani ya siku moja.

Marekani imetajwa kuongoza katika orodha ya mataifa ambayo yamerekodi maambukizi mengi zaidi, nchi ya Afrika Kusini inashikilia nafasi ya tano miongoni mwa mataifa hayo, ikiwa na maambukizi 350,879.

**Mkoa wa Gauteng nchini Afrika Kusini iliyo na miji ya Johannesburg na Pretoria, ndio kitovu kipya cha mlipuko huo.**

Hali nchini Afrika Kusini inatizamwa kama ishara ya changamoto ambayo huenda ikazikumba nchi ambazo zina vifaa haba vya huduma za afya.

Afrika Kusini ndilo taifa la kwanza la barani Afrika kuwa na idadi ya juu zaidi ya maambukizi kiasi cha kuorodheshwa miongoni mwa nchi zilizoathiriwa sana, ikishika nafasi ya tano baada ya Marekani, Brazil, India na Urusi.

Mkoa wa Gauteng nchini Afrika Kusini iliyo na miji ya Johannesburg na Pretoria, ndio kitovu kipya cha mlipuko huo.

Robo ya idadi jumla ya raia milioni 57 wa Afrika Kusini ni wakazi wa mkoa huo, huku wengi wakiishi katika mazingira ya msongamano wa watu.

Wakfu wa Askofu wa zamani, Desmond Tutu na ambaye pia ni mshindi wa tuzo ya amani ya Nobel pamoja na mke wake Leah, umeonya kwamba tatizo la Afrika Kusini ni raia wengi kutotilia maanani masharti ya WHO ya kuepusha kusambaa kwa virusi vya corona.

Katika bara la Asia, India imerekodi idadi ya juu zaidi ya maambukizi ya corona ndani ya siku moja yapatayo 38,902, hivyo kuifanya idadi ya walioambukizwa kuongezeka na kufikia watu 1, 077,618.

Wakati huo huo, China imethibitisha visa vipya 13 vya maambukizi ya virusi hivyo, kaskazini magharibi mwa mji wa Urumqi. Nayo Korea Kusini kwa siku ya pili mfululizo imeripoti maambukizi ya chini ya watu 40.

Mlipuko wa virusi hivyo eneo la Urumqi, ndio mlipuko wa hivi karibuni nchini China, baada ya taifa hilo kuudhibiti usambaaji wa virusi hivyo Machi, mwaka huu.

Idadi ya watu walioambukizwa ulimwenguni kote imefikia watu milioni 14.2. Watu milioni 3.7 miongoni mwao wakitokea Marekani, zaidi ya milioni mbili kutoka Brazil na zaidi ya milioni moja kutoka India.

Kulingana na takwimu za Chuo Kikuu cha Johns Hopkins, idadi ya watu waliofariki duniani kote kutokana na ugonjwa wa corona ni 601,549.

Marekani inaongoza idadi hiyo ikiwa imerekodi vifo 140, 119, ikifuatwa na Brazil ambayo imerekodi vifo 78,772, Uingereza imerekodi vifo 45,358 na nchini Mexico vifo 38,888. **DW**



Baadhi ya viongozi wa Umoja wa Ulaya (EU), wakiwa katika mkutano wa umoja huo mjini Brussels kuhusu bajeti ya kusaidia nchi zilizoathiriwa na ugonjwa wa virusi vya corona. **PICHA: REUTERS**

## Mpigania haki za Wamarekani weusi afariki

**WASHINGTON,** Marekani

JOHN Robert Lewis, shujaa wa kupigania haki za kiraia kwa ajili ya Wamarekani Weusi na Mwakilishi wa muda mrefu katika Baraza la Wawakilishi Marekani, amefariki dunia akiwa na umri wa miaka 80.

Mwakilishi huyo maarufu amefariki mwishoni mwa wiki baada ya mwaka mmoja wa kupambana na saratani iliyokuwa imepevuka.

John Lewis aliibuka kuwa mashuhuri kama kiongozi wa kipindi cha sasa aliyeshiriki katika harakati za haki za kiraia miaka ya 1950 na 1960.

Akiwa na umri wa miaka 23, alifanya kazi karibu sana na Mchungaji Martin Luther King, Jr. na alikuwa pekee yuko hai kama mzungumzaji mkuu wakati wa maandamano ya mwaka 1963 mjini Washington ambako King alitoa hotuba yake maarufu "I Have a Dream" (Nina Ndoto).

Wakati wa mkutano huo wa kihistoria, Lewis aliwakumbusha Wamarekani juu ya nguvu za harakati za haki za kiraia.

"Kwa nguvu ya madai yetu, ari yetu, na idadi yetu, tutaondoa ubaguzi katika eneo la Kusini na tutawunganisha wananchi kwa nguvu za Mungu na demokrasia," alisema Lewis wakati wa uhai wake. **VOA**

## Corona yaua wabunge, 25 waambukizwa

**ANTANANARIVO,** Madagascar

WABUNGE wawili nchini Madagascar wamefariki kutokana na ugonjwa wa virusi vya corona, huku wabunge wengine 25 wakiambukizwa virusi hivyo, tangu kisa cha kwanza kilipothibitishwa katika kisiwa hicho Machi, mwaka huu.

Hadi jana Madagascar imeripoti wagonjwa 5,080 waliothibitishwa kuambukizwa ugonjwa huo, huku vifo vikifikia 37.

Kulingana na taarifa zilizoripotiwa na vyombo vya habari, hali ya dharura ya kiafya imetangazwa nchini humo tangu Machi, mwaka huu na mamlaka iliweka amri ya kutotoka nje katika mji mkuu ili kuzuia kusambaa kwa virusi hivyo.

Rais wa Taifa hilo, Andry Rajoelina kwenye taarifa yake alisema: "Naibu mmoja alifariki. Seneta mmoja pia alifariki. Baada ya kufanyiwa vipimo, wabunge 11 walikutwa na corona. Katika bunge la seneti watu 14 wakiwamo maofisa na mawakala wa viongozi hao walipatikana na virusi hivyo". Hata hivyo, Rais Rajoelina hakusema ni lini wabunge hao walifariki na wala hakuwataja majina.

Rajoleina pia alisema kwamba yeye na familia yake wamekuwa wakinywa dawa ya mitishamba ya Covid Organics inayodaiwa kutibu virusi hivyo ambayo ilizinduliwa Aprili, licha ya onyo kutoka kwa Shirika la Afya Duniani (WHO) kwamba haijaidhinishwa kutumika.

"Ni kweli kwamba nimewasiliana na walioambukizwa . Nimeingia katika hospitali zinazowatibu wagonjwa wa corona. Niko salama", alisema Rajoleina na kuongeza:

"Sina virusi vya corona hata kidogo. Sina dalili. Namshukuru Mungu. Nafuata maagizo niliojiwekea, lakini zaidi ya yote mimi na wapenzi wangu mke wangu na watoto wangu, tunakunywa na kufuata maagizo ya dawa yetu ya mitishamba" **BBC**

## UN yaonya machafuko Afrika ya Kati

**BANGUI,** Afrika ya kati

UMOJA wa Mataifa (UN) umetoa wito kwa serikali ya Jamhuri ya Afrika ya Kati na mataifa jirani kuchukua hatua za kupambana na tishio la muda mrefu katika eneo hilo, hasa katika kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu.

Wataalam wa UN wanaohusika na kuchunguza vikwazo vya silaha katika Jamhuri ya Afrika ya Kati walibaini kurudiwa tena kwa mapigano, haswa Kaskazini Mashariki, yaliyochochewa na kuwasili kwa washambuliaji na silaha kutoka nje ya nchi kuja kuongeza nguvu makundi ya waasi.

Hali hiyo imetokea baada ya kukutwa kwa vitambulisho vya wapiganaji raia wa mataifa ya Tchad na Sudan waliouawa ambao ni kutoka kundi liitwalo Kikosi cha Umma kwa ajili ya uzawa mpya wa Jamhuri ya Afrika ya Kati katika shambulio la Birao Februari, mwaka huu. **RFI**

## HABARI MICHEZO

# ALVES AUNGANA NA MESSI KUIPONDA BARCA




**SAO PAULO,** Brazil

LIONEL Messi ni "binadamu tu" na anahitaji sapoti kutoka kwa Barcelona kama timu inataka kuwa na mafanikio zaidi, kwa mujibu wa mchezaji mwenzake wa zamani, Dani Alves.

Messi alizungumza kwa hasira Alhamisi baada ya Barca kupoteza kwa kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Osasuna na Madrid wakawafunga Villarreal 2-1, na kulitwaa taji la LaLiga.

Nyota huyo wa Argentina aliwaonya Barca wanaweza kuondolea na Napoli kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kama hawataweza kuimarisha kiwango chao na alidai mashabiki tayari "wamepoteza uvumilivu". Dani Alves anafikiri Messi anaelewa vizuri tu ni sehemu gani klabu hiyo inakosea kwa sasa, akiwa amefurahia mafanikio kwa kipindi cha miaka 16 aliyocheza hapo Camp Nou.

"Leo ni mshindi wa asili," alisema nyota huyo wa Brazil akiiambia redio Catalunya.

"Hapendi kupoteza. Wakati timu inapopoteza, ni kawaida kwake kuwa na hasira, mara zote anataka kushinda. Kama ilivyokwa upande wangu. Mara zote tunataka kushinda."

Dani Alves ameshinda mataji makubwa 23 pamoja na Messi, ikiwamo mara sita ya ligi na matatu ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, wakati akicheza pale Barca.

Sasa mlinzi huyo wa pembeni anayekipiga pale Sao Paulo anafikiri kikosi cha sasa cha Quique Setien ni kama "timu nyingine" bila ubora wa nyota kama ilivyokuwa kipindi chao.

"Kile kinachoonekana kwa Barca hii ni kukosa utambulisho wake kama ilivyokuwa enzi za Ronaldinho au Barca yetu," alisema.

# Cazorla aondoka rasmi LaLiga

**VILLARREAL,** Hispania

VILLARREAL imethibitisha Santi Cazorla ataondoka klabu hiyo ya LaLiga baada ya mchezo wa jana Jumapili dhidi ya Elbar.

Cazorla alikuwa na mchango mkubwa kwa timu hiyo tangu alivyorudi kuichezea kwa mara ya tatu wakati akirejea dimbani mwaka 2018 baada ya kuumia vibaya kisigino cha mguu.

Kiungo huyo mshambuliaji mwenye umri wa miaka 35, ambaye hakucheza soka kwa siku 636, baada ya kurudi uwanjani amefunga mabao 11 na kutoa pasi za mwisho tisa msimu huu.

Cazorla jana Jumapili alicheza mchezo wake wa mwisho kwenye ligi hiyo, huku akiwa anahusishwa na mpango wa kwenda klabu ya Al Sadd ya Qatari – inayonolewa na nahodha wa zamani wa Barcelona, Xavi.

Pia imeripotiwa kwamba, Cazorla anaweza kwenda kwenye benchi la ukocha katika klabu yake ya zamani ya Arsenal, lakini uwezekano wa kwenda Qatar unaonekana kuwa mkubwa zaidi kwa mchezaji huyo ambaye mwaka jana aliitwa kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya Hispania.

Cazorla aliiambia Televisheni ya Villarreal: "Villarreal imenipa kila kitu. Wakati nilipokuwa na umri wa miaka 18, walinipa ujasiri kwa kuniamini.





# Simeone: Hakutakuwa na maajabu usajili Atletico

**MADRID,** Hispania

DIEGO Simeone ana mtazamo wazi kabisa namna Atletico Madrid wanavyoweza kufanya katika dirisha la usajili linalokuja.

Atleti ni kama hawana uwezo wa kupigania taji lolote msimu huu, lakini wanauhakika wa kumaliza kwenye nne bora katika msimamo wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga na maana yake watafuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Wakati Simeone hatarajii kufanya usajili mkubwa kuelekea msimu wa 2020-21 kutokana na athari ya mlipuko wa virusi vya corona, tayati anajua nini kipya anachokitaka kuongeza hapo kwenye dimba la Wanda Metropolitano.

"Tunaendelea kuzungumza na Miguel (Angel Gil, Ofisa Mtendaji Mkuu) na Andrea (Berta, Mkurugenzi wa michezo) kuhusu nini tunachohitaji na matarajio tuliyonayo," alisema Simeone.

"Tuko wazi kabisa kuhusu kile tunachotafuta. Tuna timu inayokua, watu wapya ambao watatakiwa kuwa hapa msimu ujao.

"Katika dirisha la usajili, tuna uhakika hakutakuwa na usajili mkubwa, hivyo tutaangalia wapi kwa kujiimarisha zaidi kwa ajili ya kupambana kwenye mashindano yote msimu ujao."

Atleti hawajafungwa katika mechi 17 kwenye mashindano yote na wameshinda michezo saba kati ya 10 tangu LaLiga iliporudi Juni, mwaka huu.

Pia wamefuzu hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na watacheza dhidi ya RB Leipzig, baada ya jana Jumapili kumaliza msimu wa LaLiga kwa kucheza mchezo wa mwisho dhidi ya Real Sociedad.

HABARI MICHEZO

# Guardiola abwatukia nyota wake Man City

**LONDON,** England

PEP Guardiola anajua "hahitaji akili kubwa" kutambua kwamba Manchester City lazima iimarike ili iweze kuiondoa Real Madrid kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

City ilianza wiki hii kwa ushindi wa rufaa yao baada ya Makahama ya Usuluhishi wa Michezo (CAS), kuwafutia adhabu ya kufungiwa kushiriki mashindano ya Ulaya kwa miaka miwili waliyopewa na UEFA, kutokana na kuvunja sheria ya haki ya usawa kwenye matumizi ya fedha za usajili wa wachezaji.

Dimbani habari ilikuwa tofauti, kwani Guardiola alishutumu kiwango cha wachezaji wake wakati wakipokea kipigo cha mabao 2-0 kwenye mchezo wa nusu fainali ya Kombe la FA kutoka kwa Arsenal.

Licha ya kushinda taji la EFL Machi, City inakabiliwa na kibarua cha kuiondoa Madrid kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16.

Katika mchezo wa kwanza, City waliibuka na ushindi wa mabao 2-1, hivyo wanahitaji ushindi kwenye mchezo wa pili ili kufuzu robo fainali wakati watakapokutana na Madrid Agosti 7, mwaka huu.

Mshindi wa mchezo huo atafuzu robo fainali ambapo atakutana kati ya Juventus au Lyon.

"Sitakiwi kuwaambia. Wanajua, nini kinatakiwa kwa sasa," alisema Guardiola, ambaye pia alibainisha wachezaji wake walistahili kufungwa, wakati wakiibuka na ushindi wa 2-1 katikati ya wiki dhidi ya Bournemouth waliopo kwenye hatari ya kushuka daraja.

"Tunajua ubora tunaotakiwa kuwa nao tukiwa kwenye hatua hii. Haihitaji akili kubwa kujua kwamba tunahitaji kuimarika wakati tunakwenda kuwavaa Madrid, kwani bila hivyo hatutaweza kufuzu."





# KOCHA MILAN AMTULIZA MZUKA IBRAHIMOVIC

**MILAN,** Italia

STEFANO Pioli amesema alihitaji kumtuliza Zlatan Ibrahimovic baada ya nyota huyo wa Milan kuonekana amekasirika wakati akitolewa nje kwenye mchezo dhidi ya Bologna.

Ibrahimovic alitoa pasi ya mwisho kabla ya kutolewa nje wakati Milan wakiibuka na ushindi wa 5-1 kwenye mchezo huo wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, pale katika dimba la San Siro, Jumamosi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 38, alionekana kukasirika wakati akitolewa nje, lakini kocha Pioli amesema aliweza kumtuliza Ibrahimovic.

"Alisema kitu fulani, lakini kiukweli sikuelewa. Ni kawaida," alisema akiambia DAZN. "Nilitakiwa kumtuliza, kwani najua kila mmoja anatakiwa kuwa mtulivu."

Alexis Saelemaekers, Hakan Calhanoglu, Ismael Bennacer, Ante Rebic na Davide Calabria kila mmoja aliifungia bao moja Milan.

Wakiwa wapo nafasi ya sita kwenye msimamo wa Serie A, Milan haijafungwa katika mechi tisa tangu kurudi kwa ligi hiyo baada ya mlipuko wa virusi vya corona na Pioli ana furaha na kiwango cha kikosi chake.

"Timu ipo viruri na inacheza vizuri zaidi. Tumecheza kwa kiwango cha kuvutia karibia katika kila mchezo, tupo vizuri," alisema.

# *Zidane: Mimi si spesho Madrid, nina bahati tu*

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane amesisitiza yeye si 'special one', akisema ana bahati tu anapokuwa kwenye benchi kuinoa Real Madrid.

Zidane ameiongoza Madrid kutwaa taji la LaLiga msimu huu likiwa kombe lake la 11 kama kocha kwa miamba hao wa Hispania.

Lakini Mfaransa huyo alikataa kauli kwamba yeye ni 'special one' jina ambalo Jose Mourinho alikuwa akilitumia awali kujitambulisha yeye mwenyewe.

"Hapana, hapana. Sihisi hivyo. Najihisi tu ni mtu mwenye bahati kuwa hapa na wachezaji kila siku," alisema Zidane akiwaambia waandishi wa habari.

"Kuwa na klabu, ndilo jambo ninaloliona kuwa bahati, na ndio maana nafurahia hilo kila siku. Kwa sababu siku moja hali hiyo itamalizika, kama ambavyo ilishawahi kutokea."

"Ndio maana nafurahia na kujikita kwa kile ambacho natakiwa kukifanya kwa wakati uliopo."

Taji hilo la Madrid kwenye LaLiga lilikuwa la kwanza kwao tangu msimu wa 2016-17, wakati Cristiano Ronaldo alipowaongoza kulitwaa kwa mara ya mwisho.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA: AUBAMEYANG SASA ANAWEZA KUBAKI

Kwa uhakika kabisa nina furaha na najisikia fahari juu ya wachezaji wangu...

**LONDON,** England

MIKEL Arteta anaamini Pierre-Emerick Aubameyang "anaweza kushawishika" kubaki Arsenal, lakini amebainisha kwamba kushinda taji la FA kunaweza kuimarisha nguvu za klabu hiyo kujaribu kumbakiza kwa kumpa mkataba mpya.

**Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, mkataba wake wa sasa pale Arsenal unamalizika kipindi cha majira ya joto kinachokuja na ESPN ili bainisha mapema mwezi huu kwamba, anataka kuongezea miaka mitatu na mshahara wa pauni 250,000 kwa wiki.**

Majadiliano yatachukua nafasi zaidi kama 'Washikabunduki' hao watafuzu kucheza mashindano ya Ulaya msimu ujao, na sasa ushindi wa Jumamosi wa mabao 2-0 kwenye mchezo wa nusu fainali ya Kombe la FA dhidi ya Manchester City unaweza kumshawishi zaidi.

Aubameyang alifunga mabao yote mawili dhidi ya kikosi hicho cha kocha, Pep Guardiola na Arteta alisema baada ya mchezo huo: "Namna nilivyomuangalia yeye wakati nazungumza naye, anaonyesha kushawishika.

"Lakini kama ataweza kuona mafanikio zaidi na muelekeo tulionao, nafikiri atakuwa chanya zaidi kusaini mkataba mpya na sisi."

Aubameyang aliipa Arsenal bao la kuongoza dakika ya 17 na la pili zikiwa zimesalia dakika 18 mpira kumalizika, akiwaacha vijana hao wa Guardiola wakiwa hawana namna, na kuzima matumaini yao ya kushinda mataji matatu msimu huu, baada ya kufanya hivyo msimu uliopita.

Arsenal, yenye rekodi ya kushinda taji la FA mara 13, watacheza dhidi ya Chelsea au Manchester United kwenye fainali Agosti Mosi mwaka huu ambazo zilikutana jana.

Ukiangalia kwenye msimamo wa ligi, Arsenal wapo nafasi ya tisa, lakini Arteta mwenye umri wa miaka 38, ana kila sababu ya kubeba taji hilo ikiwa ni kwa mara yake ya kwanza akiwa kocha mkuu.

"Kwa uhakika kabisa nina furaha na najisikia fahari juu ya wachezaji wangu," alisema Arteta.

"Wakati unapocheza na timu yenye kasi kama ile na ukapata nafasi na ukazitumia kwa umakini ni jambo zuri zaidi kwa kikosi chetu.

"Kumekuwa na muunganiko mzuri kati ya wachezaji na kwa hakika naamini wanajaribu kufanya kitu fulani kizuri zaidi kwa timu."

## ZISIKUPITE

### SETIEN NA BARCA UEFA

KOCHA aliyekalia kuti kavu pale Barcelona, Quique Setien atabakia kuiongoza timu hiyo kwenye mchezo wa pili wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya timu 16 dhidi ya Napoli, baada ya mazungumzo na rais, Josep Maria Bartomeu. ***(Evening Standard)***

### SPURS KWA PIERRE-EMILE

MPANGO wa Tottenham Hotspur kumuwania kiungo wa Southampton, Pierre-Emile Hojbjerg mwenye umri wa miaka 24 raia wa Denmark, umeongeza shaka juu ya majaliwa ya kiungo mzawa wa England, Harry Winks mwenye miaka 24, klabuni hapo. ***(Sunday Mirror)***

### GREENWOOD KUFUNGWA UTD

MSHAMBULIAJI kinda wa Manchester United, Muingereza Mason Greenwood mwenye umri wa miaka 18, atapewa mkataba mpya hapo Old Trafford ambao utamfanya alipwe mshahara wa pauni 40,000 kwa wiki - ikiwa ni miezi tisa tu tangu asaini mwingine. ***(Sun on Sunday)***

### TERRY AFIKIRIWA BRISTOL

KOCHA msaidizi wa Aston Villa, John Terry anafikiriwa na Bristol City kuwa kocha wake mkuu mpya baada ya chaguo lao la kwanza, Steven Gerrard kuipiga chini ofa ya kujiunga na timu hiyo ya daraja la kwanza. ***(Sunday Express)***

### ARSENAL YAMTAKA FERNANDES

ARSENAL ipo tayari kutoa kiasi cha pauni milioni 40 kumsajli mshambuliaji kinda wa Sporting Lisbon na timu ya Taifa ya Ureno chini ya umri wa miaka 17, Joelson Fernandes, aliyezivutia Barcelona na Juventus. ***(A Bola)***

### SANCHO SOKONI DORTMUND

KLABU ya Borussia Dortmund imeweka bei ya pauni milioni 115 kwa ajili ya kumuuza Jadon Sancho,20, lakini winga huyo wa England, anayehusishwa na Manchester United, amekataa kuondoa uwezekano wa kuondoka katika klabu hiyo ya Ujerumani. ***(Sunday Express)***

### CITY YAMUWANIA ROSA

MANCHSTER City ipo kwenye mazungumzo na klabu ya nchini Brazil ya Gremio juu ya mpango wa kumsajili kiungo Diego Rosa mwenye umri wa miaka 17 kwa pauni milioni 4.5. ***(Mail on Sunday)***

### LONGSTAFF AITESA NEWCASTLE

NEWCASTLE United watajaribu kumshawishi Matty Longstaff,20, alikubali kusaini mkataba wa muda mfupi ili kumalizia msimu baada ya kusimama kutoka na mlipuko wa virusi vya corona na atakuwa mchezaji huru baada ya ligi hiyo kumalizika. ***(Independent)***

### ANCELOTTI KUIJENGA EVERTON

KOCHA wa Everton, Carlo Ancelotti, anajiamini ataungwa mkono na bodi ya klabu kwenye dirisha la usajli la kipindi hiki cha majira ya joto, baada ya kusema kikosi chake kinahitaji kuimarishwa. ***(Sky Sports)***

### ZENIT YAMTAKA LOVREN

ZENIT St Petersburg wapo tayari kutoa ofa ya pauni milioni tisa kwa ajili ya kumsajili mlinzi wa Liverpool, Dejan Lovren,31, lakini mabingwa hao wa Ligi Kuu ya England wanataka pauni milioni 15 ili kumuachia nyota huyo wa kimataifa wa Croatia. ***(Mail on Sunday)***

HABARI MICHEZO

## Kocha Singida Utd aulaumu uongozi

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Singida United, Ramadhani Nswanzurwimo amesema kwa mazingira magumu ya timu hiyo ndiyo yaliyowasababishia kufanya vibaya msimu huu na kushuka daraja.

Singida United imekuwa timu ya kwanza Ligi Kuu kushuka daraja baada ya kujikusanyia alama 18 tu katika mechi 36 wakati huu zikiwa zimebaki mechi mbili kabla ya msimu kumalizika.



Nswanzurwimo aliliambia gazeti hili jana kuwa, utendaji wa viongozi pamoja na kukosa fedha ya kuwalipa mishahara wachezaji wao ndiko kulikosababisha timu hiyo kutofanya vizuri.

Alisema uongozi haukusimama imara kujenga kikosi chao na kufanya maandalizi mazuri mwanzoni mwa msimu kabla ya kuanza ligi.

"Kuna mambo mengi sana yaliyofanya timu kushuka daraja, ikiwamo utendaji mbovu wa viongozi, kutofanya usajili mzuri, kuwaondoa wachezaji wazuri na kuwapeleka timu zingine," alisema.

## Simba Queens kusaka tena 3 J'5

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kutoa kipigo cha mabao 3-1 dhidi ya Kigoma Sisters, timu ya wanawake ya Simba Queens keshokutwa, Jumatano itashuka tena dimbani safari hii ikiwa mwenyeji wa Mlandizi Queens kwenye Uwanja wao wa Mo Simba Arena, Bunju jijini Dar es Salaam.

Simba Queens ambayo ipo kileleni ikiwa na pointi 44 baada ya kucheza mechi 17 wakati huu wakiwa wamebakiza mechi tano kabla ya kuhitimisha msimu juzi ilionyesha kandanda la kuvutia katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma.

Katika mchezo huo ambao Malkia hao wa Simba waliutawala kwa sehemu kubwa, walipata mabao yote matatu kipindi cha kwanza yakifungwa na Mwanahamisi Omari dakika ya 10 na Oppa Clement aliyetupia mawili dakika ya 16 na 40.

Bao pekee la kufutia machozi la Kigoma Sisters liliwekwa kimiani na Kadosho Shaban kwa mkwaju wa penati dakika ya 89.

Kikosi hicho cha Malkia wa Simba kinachonolewa na Musa Hassan 'Mgosi', kiliondoka Kigoma jana kurejea jijini Dar es Salaam tayari kwa maandalizi ya kuivaa Mlandizi Queens.

# MWADUI YAICHONGEA MTIBWA KWA YANGA

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Klabu ya Yanga, Mbelgiji Luc Eymael, amekerwa na sare aliyoipata juzi dhidi ya Mwadui FC katika Uwanja wa Taifa na sasa anaelekeza nguvu zake kwenye michezo iliyobaki ili kuhakikisha wanamaliza katika nafasi ya pili msimu huu.

Tayari Simba imetwaa ubingwa huo huku kila timu ikiwa imebakiza mechi mbili kabla ya msimu kumalizika, wakati Yanga yenye alama 68, ikiwania nafasi ya pili sambamba na Azam FC iliyojikusanyia pointi 65 kabla ya mechi yao ya jana dhidi ya Lipuli FC.

Akizungumza na gazeti hili jana, Eymael alisema hajafurahishwa na sare waliyoipata juzi walipokutana na timu ya Mwadui na kufungana bao 1-1.

**"Najipanga kwa ajili ya kuhakikisha nashinda michezo iliyopo mbele yetu tushike nafasi ya pili," alisema Eymael.**

Kocha huyo alisema kwa sasa anaelekeza nguvu zake zote kwenye mchezo ujao dhidi ya Mtibwa Sugar ambao utapigwa keshokutwa katika Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro kabla ya kuhitimisha ligi hiyo msimu watakapoifuata Lipuli ya Iringa.

Alisema anauheshimu mchezo huo na kuahidi kufanyia marekebisho upungufu wote ambao ameubaini katika mchezo wao uliopita.

"Ninaupa umuhimu mkubwa mchezo huo, lengo langu ni kupata pointi tatu tumalize ligi tukiwa tumeshika nafasi ya pili," alisema.

Alisema msimu huu una ushindani mkubwa na kudai msimu ujao atarudi na nguvu mpya ikiwa ni pamoja na kuongeza nguvu katika kikosi chake hicho.

Alisema ataziba mapengo katika nafasi ambazo ameziona zina upungufu ili msimu ujao Yanga ishike nafasi ya juu.

BONGO FLEVA...



Wanafunzi wa Shule ya Msingi, St Anne Marie Academy ya Mbezi Kimara kwa Msuguri jijini Dar es Salaam, wakiwaburudisha kwa nyimbo za Bongo Fleva wageni waliohudhuria kwenye mahafali ya 12 ya kidato cha sita shuleni hapo mwishoni mwa wiki. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# *Makata kuwasilisha ripoti Dodoma FC*

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Dodoma FC, Mbwana Makata, amesema leo atakabidhi ripoti yake kwa uongozi wa klabu hiyo ambayo imebeba mapendekezo ya usajili wa timu hiyo yakilenga kufanyika maboresho madogo ili kukiimarisha kikosi chake kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Dodoma imepanda Ligi Kuu baada ya kumaliza msimu ikiwa vinara wa Kundi A la Ligi Daraja la Kwanza kwa kujikusanyia pointi 51 na juzi kutwaa ubingwa huo kwa kumfunga kinara wa Kundi B, Gwambia FC katika fainali ya ligi hiyo kwa ushindi wa bao 1-0 mchezo uliopigwa kwenye dimba la Azam Complex, Chamazi.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Makata alisema hatafanya maboresha makubwa katika kikosi chake na atabaki na asilimia kubwa ya wachezaji waliyoipandisha timu hiyo.

Alisema ataongeza nyota wapya ambao wana uzoefu na Ligi Kuu ili kusaidia timu yao hiyo kutoa ushindani mkubwa katika soka la Tanzania.

"Maboresho ya kikosi yatafanyika kwa ajili ya kuongeza baadhi ya wachezaji, tutaongeza nguvu katika baadhi ya nafasi ambazo zilikuwa na upungufu, waje kusaidiana waliopo," alisema Makata.

Alisema wamekuja kuleta ushindani, na wanafanya usajili kuimarisha kikosi chao ili kufanya vizuri katika Ligi Kuu na hawaendi kushiriki na kurudi chini kama ilivyokuwa timu zingine kucheza msimu mmoja na kushuka.

"Kikubwa ni kuendelea kupewa sapoti kutoka kwa wananchi pamoja na wadau wa soka, baada ya timu kupanda, sapoti yao ni muhimu katika kila nafasi kuanzia usajili pamoja na maandalizi ya timu kabla ya kucheza Ligi Kuu," alisema Makata.

# Michezo

Jumatatu Julai 20, 2020

Nipashe




‘Aubameyang sasa anaweza kubaki’ UKURASA 22

**MWALI WETU...**



Nahodha Msaidizi wa Simba, Mohamed Hussein ‘Tshabalala’, akinyanyua juu Kombe la Ligi Kuu baada ya timu hiyo kuichapa Alliance FC mabao 5-1 kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Taifa jana. Simba ambayo ilishajihakikishia ubingwa, mechi hiyo ilikuwa ya mwisho kwao katika uwanja wa nyumbani kabla ya kufuata Coastal Union ya Tanga kisha Jumapili kuhitimisha msimu na Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Ushirika mjini Moshi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Kagere anusa rekodi Simba ikipiga mkono*

## ●●● Azam nayo ngoma nzito kuishusha Yanga, yang’ang’aniwa na Lipuli Samora...

**Na Adam Fungamwango**

MABAO mawili ya kinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Mnyarwanda Meddie Kagere, Luis Miquissone raia wa Msumbiji, Mkongomani Deo Kanda na Mtanzania Said Ndemla, jana yaliiwezesha Simba kutoka kipigo kizito cha mabao 5-1 dhidi ya Alliance FC ya Mwanza na kuendelea kuiweka kwenye mazingira magumu ya kucheza Ligi Kuu msimu ujao.

**Kwa kipigo hicho, Alliance inabaki na pointi zake 41, ikibakisha mechi mbili, huku ikishika nafasi ya 17, ikiwa ya tatu kutoka mkiani.**

Kwenye mechi hiyo iliyochezwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, Simba ilianza mechi kwa kasi na kukosa mabao mawili ya wazi, likiwamo shuti la Luis Miquissone kugonga mwamba wa juu na kurudi uwanjani.

Ilikuwa ni dakika ya 23 Simba ilipata bao la kwanza kupitia kwa Kagere kwa mkwaju wa penalti hilo likiwa bao lake la 21 msimu huu.

Penalti hiyo ilitokana na kipa wa Alliance, John Mwenda kumkamata miguu, Miquissone, aliyekuwa amemlamba chenga na kutaka kuuweka mpira ndani ya wavu.

Dakika ya 30, nusura Miquissone aweke bao la pili, lakini alipiga shuti dhaifu ambalo kabla halijaingia wavuni kipa Mwenda akiwa hayupo golini, uliokolewa na beki Erick Murilo.

Makosa yaliyofanywa na kiungo Jonas Mkude kuuchezea mpira, yalisababisha Alliance kurudisha bao, baada ya kunyang’anywa kirahisi na mpira kumfikia Martin Kiggi aliyeuweka mpira huo ndani ya wavu dakika ya 36.

Dakika moja kabla ya timu kwenda mapumziko, Kagere kwa mara nyingine aliiweka mpira ndani ya wavu na kuipatia Simba bao la pili, akiunganisha krosi safi kutoka kwa Francis Kahata, baada ya kazi kubwa iliyofanywa na Miquissone na kumfanya kufikisha mabao 22 kwenye ligi, akiendelea kuwa kinara huku akibakisha bao moja kufikia rekodi yake ya msimu uliopita ya mabao 23.

Miquissone alisahihisha makosa yake dakika ya 64 kwa kupachika bao maridadi, alipopiga shuti la kiufundi lililokatika mithili ya mwezi mchanga na kumshinda kipa Mwenda, mpira ukajaa wavuni.

Kama vile haitoshi, Simba ambayo ilichezesha kikosi chake kamili, tofauti na kile kilichocheza dhidi ya Mbao FC na kuchapwa mabao 3-2, ilipata bao la nne dakika ya 75 lililofungwa na mtokea benchi, Kanda, ambaye alifunga kwa kifua, baada ya krosi maridadi ya Kegere.

Mtokeo benchini mwingine Said Ndemla alikamilisha karamu ya mabao dakika tatu kabla ya mechi kukamilika alipofunga bao la tano kutokana na pande la mtokea benchini mwenzake, Hassan Dilunga.

Kwa matokeo hayo Simba inafikisha pointi 84, huku tayari ikiwa imeshatwaa ubingwa.

Matokeo ya mechi zingine ni Lipuli kung’ang’aniwa shati nyumbani dhidi ya Azam kwa kufungana bao 1-1 kwenye Uwanja wa Samora mkoani Iringa, huku JKT Tanzania ikiwa Uwanja wa Jamhuri Dodoma ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Mbao FC.

Matokeo hayo ya Azam yanaifanya kufikisha pointi 66, mbili nyuma ya Yanga ambayo itashuka dimba la Jamhuri keshokutwa, Jumatano kuivaa Mtibwa Sugar kwenye mchezo wao wa 37.

# TFF yageukia lala salama Ligi Kuu

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF)kupitia kwa Bodi ya Ligi nchini (tplb), limesema linaongeza umakini kwenye mechi za kuelekea mwishoni mwa msimu wa Ligi Kuu Bara ili kusiwe na matukio ya upangaji matokeo.

Mwenyekiti wa TPLB, Steven Mguto, amesema wanaongeza uangalizi kwenye mechi zilizobaki za Ligi Kuu, ili kupatikana matokeo halali kutokana na timu nyingi kuwa katika hatari ya kushuka daraja, huku kila moja ikitaka kujinasua kwenye janga hilo.

“Uangalizi utaongezeka, tutaongeza wajumbe kwenye michezo yote ili matokeo yote yawe halali. Uchunguzi umeonyesha kunapokuwa na waangalizi, basi kunakuwa na uhakika zaidi wa matokeo halali,”alisema Mguto.

Mwenyekiti huo alisema mechi zilizobaki ni chache, hivyo wana uwezo kupeleka wajumbe kote, kwa sababu watapeleka pale tu ambapo wanaona mechi hiyo inaweza kuwa na matokeo chanya kwa timu zote. Katika kile kinachoonekana kama kauli ya Mguto imeanza kufanyiwa kazi, kwenye mechi zote saba zilizochezwa Jumamosi wiki hii, hakuna timu yoyote iliyoshinda nyumbani.

Yanga ikiwa nyumbani Uwanja wa Taifa ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Mwadui, Biashara United nayo ikapata matokeo kama hayo Uwanja wa Karume mjini Musoma dhidi ya Coastal Union, Kagera Sugar ikachezea kichapo cha 2-1 Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba dhidi ya Polisi Tanzania, Mtibwa Sugar ikiwa CCM Gairo, ikachapwa bao 1-0 dhidi ya KMC, Namungo, katika Uwanja wa Majaliwa mjini Lindi ikalazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Prisons, Ndanda ikafungwa nyumbani Nangwanda Sijaona mjini Mtwara bao 1-0 dhidi ya Mbeya City, na Ruvu Shooting ikiwa Mabatini Mlandizi mkoani Pwani ikakubali kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya vibonde, Singida United.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >